


# Ulinzi wa Wanawake Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia Tanzania

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika(WiLDAF)

# Ulinzi wa Wanawake Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia Tanzania

WiLDAF

Novemba, 2011
Dar es Salaam
Tanzania

Kitabu hiki kimeandaliwa na kuchapishwa na:

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)
Mikocheni "A", Mtaa wa Chwaku
S. L. P 76215, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2701995
Barua pepe: wildaf_tanzania@yahoo.com
info@wildaftanzania.org
Tovuti: www.wildaftanzania.org

© WiLDAF Tanzania, 2011

ISBN 978-9987-9246-2-2

Katuni na Usanifu: Marco Tibasima (marcotibasima@yahoo.com)

Kitabu hiki kimetolewa kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID).
Hata hivyo yaliyomo kwenye kitabu hiki siyo lazima yawakilishe maoni na mitazamo ya USAID, WiLDAF inawajibika kwa mapungufu yoyote yatakayojitokeza katika kitabu hiki.

# SHIRIKA LA WiLDAF

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), ni mtandao wa mashirika na watu binafsi katika Bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupigania haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushiriki na ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilo jiendesha kwa faida.

WiLDAF Tanzania ina njozi ya kuona jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Misheni yake ni kujenga mtandao imara kwa ajili ya kukuza heshima kwa haki za binadamu za wanawake kupitia utetezi, usambazaji na uangalizi wa vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha sheria na maendeleo.

# YALIYOMO

**Shukrani** ........ iv

**Dibaji** ........ v

**Utangulizi** ........ vi

**Sura Ya Kwanza: Jinsia Na Haki Za Binadamu/ Mwanamke** ........ 1

1.1 Utangulizi
1.2 Dhana Ya Jinsi Na Jinsia
1.3 Jinsia Na Haki Za Binadamu
1.4 Maana Ya Haki Za Binadamu
1.5 Aina Ya Haki Za Binadamu
1.6 Utambuzi Na Ulinzi Wa Haki Za Binadamu Kisheria
1.7 Misingi Ya Haki Za Binadamu Kwa Mujibu Wa Tamko La 1948
1.8 Utambuzi Wa Haki Za Wanawake

**Sura Ya Pili: Ukatili Wa Kijinsia, Aina, Chanzo, Sababu Na Matokeo Yake** ........ 5

2.1 Maana Ya Ukatili Wa Kijinsia
2.2 Aina Za Ukatili Wa Kijinsia
2.3 Sababu Na Chanzo Cha Ukatili Wa Kijinsia
2.4 Viashiria Vya Ukatili Dhidi Ya Wanawake
2.5 Matokeo Ya Ukatili Wa Kijinsia

**Sura Ya Tatu: Mahusiano Kati Ya Ukatili Wa Kijinsia, Umaskini, Mila Na Ukimwi Pamoja Na Athari Zake** ........ 8

3.1 Utangulizi
3.2 Mahusiano Kati Ya Ukimwi Na Ukatili Wa Kijinsia
3.3 Sababu Kuu Za Masuala Ya Jinsia Na Ukimwi
3.4 Mahusiano Kati Ya Umaskini Na Ukatili Wa Kijinsia
3.5 Athari Za Ukatili Wa Kijinsia

**Sura Ya Nne: Ulinzi Wa Haki Za Wanawake Kwa Mujibu Wa Mikataba Ya Kimataifa** ........ 11

4.1 Utangulizi
4.2 Tamko La Kimataifa La Haki Za Binadamu La 1948
4.3 Mkataba Wa CEDAW wa 1979
4.4 Mkataba wa Maputo wa 2003
4.5 Haki Za Wanawake Kwa Mujibu Wa Mkataba Wa Maputo.
4.6 Azimio La Beijing La Masuala Ya Jinsia La 1995

**Sura Ya Tano: Ulinzi Wa Haki Za Wanawake Kwa Mujibu Wa Katiba Ya Tanzania** ........ 15

5.1 Utangulizi
5.2 Haki Na Wajibu Mbalimbali Kwa Mujibu Wa Katiba Ya Tanzania

**Sura Ya Sita: Ulinzi Wa Haki Za Wanawake Kwa Mujibu Wa Sheria Mbalimbali Za Tanzania** ........ 19

6.1 Utangulizi
6.2 Sheria Ya Ndoa Ya Mwaka 1971
6.3 Aina Za Ndoa Kwa Mujibu Wa Sheria
6.4 Baadhi Ya Haki Za Mwanamke Kwa Mujibu Wa Sheria Ya Ndoa
6.5 Sheria Za Ardhi Za Mwaka 1999
6.6 Sheria Ya Ajira Na Mahusiano Kazini, 2004
6.7 Sheria Ya Kuzuia Na Kupambana na Vvu Na Ukimwi Ya 2008

**Sura Ya Saba: Kitendo Cha Ukatili Wa Kijinsia Kama Kosa La Jinai........27**

7.1 Utangulizi
7.2 Sheria Ya Kanuni Za Adhabu, Sura Ya 16

**Sura Ya Nane: Vyombo Vya Usimamizi Wa Haki Dhidi Ya Ukatili Wa Kijinsia........3**
8.1 Utangulizi
8.2 Usimamizi Ngazi Ya Kimataifa
8.3 Usimamizi Ngazi Ya Kikanda - Afrika
8.4 Usimamizi Kitaifa - Tanzania

**Sura Ya Tisa: Jitihada, Mafanikio Na Changamoto za Juhudi Dhidi Ya Ukatili Wa Kijinsia........34**

9.1 Utangulizi
9.2 Jitihada Zilizofanywa Na Serikali
9.3 Jitihada Za Asasi Za Kiraia
9.4 Jitihada Zilizofanywa Na Jamii
9.5 Jitihada Za Mashirika Ya Maendeleo/Wahisani
9.6 Baadhi Ya Changamoto

**Sura Ya Kumi: Mapendekezo Ya Jumla........38**

10.1 Utangulizi
10.2 Mapendekezo Kwa Serikali
10.3 Mapendekezo Kwa Taasisi
10.4 Mapendekezo Kwa Jamii
10.5 Mapendekezo Kwa Wadau Wa Maendeleo

**Vifupisho........40**

# SHUKRANI

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, Tawi la Tanzania (WiLDAF Tanzania) linatoa shukrani za dhati kabisa kwanza kwa mbia wetu wa maendeleo USAID Tanzania kwa kufadhili utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa kitabu hiki. Kwa upendo wao mkubwa, elimu hii imeweza kuwafikia jamii pana ya watanzania na kuwafanya baadhi yao kuwa sehemu ya mchakato wa kusimamia na kutetea haki za binadamu, hususani kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.

Shirika la WiLDAF Tanzania pia linawashukuru wafanyakazi wake Anna Kulaya, Alicko Sengo na Judith Odunga kwa uandaaji wa rasimu ya kwanza ya kitabu hiki. Aidha pia inawashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na wanachama wake kwa kutoa maoni yao kwa njia mbalimbali. Shukrani za pekee ziwaendee washiriki wafuatao wa semina ya mapitio ya kitabu hiki kwa mchango wao wa kipekee, Laetitia Petro (LHRC), Ramadhani Masele (FHI 360), Juliana Laurent (CHRAGG), Allan Kajembe (CWCA), Merina Maneo (TWCWC), Festo Ntibalizi (TALAPA), Leodgard Lazarus (ANAPPCAN), Mayasa Jengo (KIU), Samwel Lyimo (ICNIC), Desderia Haule (CHRAGG), Edna Makala (HoP) Mackphason Buberwa (TAWLA).

Aidha, shukrani zetu za dhati pia kwa Bw. Clarence Kipobota (Wakili) wa Shirika la Wataalam Washauri katika Sheria na Maendeleo (LEDECO Advocates), kwa kuhariri na kuongezea maelezo mazuri katika kitabu hiki.

Shirika la WiLDAF pia linamshukuru Faith Okeyo kwa kuchapa kazi hii.

Mwisho kabisa, tunawashukuru sana Asasi za Kiraia; Jeshi la Polisi Tanzania; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Serikali ya Tanzania Kiujumla; Wahudumu wa Sekta ya Afya na wananchi wote kwa ujumla kwa kutuunga mkono na kuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia hapa nchini.

Shukrani.

**Dkt. Judith N. Odunga**
Mratibu Kitaifa.

# DIBAJI

Ukatili wa kijinsia ni kitendo chochote anachofanyiwa mtu yeyote mwanamke, mwanaume au mtoto kwa lengo la kuleta madhara ya kimwili, kingono, kiutamaduni, kisaikolojia, maumivu au hata kifo, kinachotokea katika familia au jamii.

Kwa ujumla, ukatili wa kijinsia hususan ukatili dhidi ya wanawake ni matokeo ya tofauti ya hali na mahusiano ya kimamlaka kati ya wanawake na wanaume katika familia na katika jamii. Hali hii tofauti kwa upande mwingine hubebwa na mfumo wa sheria, malezi na makuzi na hata tofauti katika kupata na kumiliki rasilimali. Pia ukatili wa kijinsia, hususan dhidi ya wanawake ni matokeo ya kuhalalishwa kwa vitendo vya kikatili kwa kisingizio cha hatua za kinidhamu ndani ya mamlaka na madaraja ya kijamii pamoja na makundi rika.

Ingawa hali hii inaruhusu mjadala, ukatili wa kijinsia umekuwa ukihusishwa na tabia na matatizo ya kisaikolojia ya watenda ukatili na wahanga wa ukatili kama vile kujitenga na jamii, kilevi, madawa ya kulevya, makuzi ya kikatili na kushindwa kujitawala. Matokeo ya vyanzo hivi ni eneo gumu linalohitaji njia zilizojengeka kupambana navyo.

Takwimu nyingi zinaainisha bayana kwamba wanawake wengi ndio wahanga wa ukatili wa kijinsia. Mathalani utafiti uliofanywa na Idara ya Takwimu mwaka 2010 kuhusu hadhi ya wanawake nchini Tanzania ulibaini yafuatayo:-

- Asilimia 39 ya wanawake wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe iwapo mke atajibishana naye.
- Asilimia 37 ya wanawake waliohojiwa wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe kwa sababu ya kuondoka nyumbani bila ya kumuaga mumewe.
- Asilimia 40 ya wanawake wanakubali kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe pale mwanamke anapozembea kuangalia watoto.
- Asilimia 30 ya wanawake wanakubali kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe iwapo atakataa kufanya tendo la ndoa.
- Asilimia 18 ya wanawake wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe ikiwa ataunguza chakula.
- Asilimia 53 ya wanawake wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe kwa sababu nyingine yeyote ile.

Kutokana na uwepo wa hali hii ambayo kwa hakika ina matokeo mabaya kwa jamii hususan wanawake na watoto. Kitabu hiki kimetungwa ili kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali ya kijinsia. Lengo lake hasa ni kuufahamisha umma maana ya ukatili wa kijinsia, vyanzo vyake, matokeo yake pamoja na njia mbalimbali za kupambana nao hasa kwa kutumia sheria za kimataifa na kitaifa zinazohusu haki na wajibu wa masuala haya.

Ni matumaini ya WiLDAF Tanzania kuwa, msomaji wa kitabu hiki atanufaika na yaliyomo na kuwa sehemu ya chachu ya mabadiliko ya kisheria, sera na tamaduni mbovu/potofu ambavyo vinaletea uwepo wa ukatili wa kijinsia katika jamii zetu.



Mh. Naomi A. M. Kaihula
Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi ya WiLDAF.

# UTANGULIZI

Kitabu hiki kinaelezea kwa kina jitihada nyingi zilizofanywa na serikali, vyombo vya kimataifa na wadau wa maendeleo zikiwamo Asasi zisizo za kiserikali na wadau wengine katika kutetea usawa wa kijinsia na haki za wanawake, hususan ulinzi wa wanawake dhidi ya ukatili.
Kitabu hiki cha ulinzi wa Wanawake Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia Tanzania kimegawanyika katika Sura Kumi.

**Sura ya Kwanza** inaelezea dhana ya Jinsi na Jinsia, Haki za Binadamu, hususan haki za binadamu za wanawake,. kwa kuainisha mahusiano ya masuala hayo ili kujenga uelewa mpana wa masuala yaliyomo katika sura zingine zinazofuata kwenye kitabu hiki.

**Sura ya Pili** inajadili ukatili wa kijinsia, aina, chanzo, sababu na matokeo yake. Aidha inaainisha kwa kirefu aina za ukatili wa kijinsia ikiwewamo ukatili wa kimwili, kisaikolojia, kingono, kiuchumi na kiafya. Inaelezea sababu na chanzo cha ukatili wa kijinsia ikiwamo mila na desturi potofu, mfumo dume, tafsiri potofu ya vitabu vya dini, wivu wa mapenzi, sera na sheria kandamizi pamoja na elimu duni. Sura hii pia imejadili viashiria vya ukatili pamoja na matokeo ya ukatili wa kijinsia.

**Sura ya Tatu** inajadili mahusiano kati ya ukatili wa kijinsia, umaskini, mila na UKIMWI pamoja na athari zake. Aidha inaainisha suala la umaskini kama chanzo na sababu kuu za masuala ya jinsia na UKIMWI. Aidha mahusiano kati ya umaskini na ukatili wa kijinsia yamebainishwa kama vile kutomiliki ardhi au mali nyingine, ukosefu wa elimu kwa wasichana, ubaguzi dhidi ya wanawake na kadhalika. Athari za ukatili wa kijinsia pia zinajadiliwa kwa kina.

**Sura ya Nne** inaelezea ulinzi wa Haki za Wanawake kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa ikiwamo Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948, Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake wa Mwaka 1979, Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Afrika (Maputo Protocol) wa mwaka 2003 na Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la Mwaka 1995 limejadiliwa.

**Sura ya Tano** inajadili Ulinzi wa Haki za Wanawake kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Aidha haki mbali mbali kwa mujibu wa Katiba pia zimejadiliwa.

**Sura ya Sita** inaelezea ulinzi wa haki za wanawake kwa mujibu wa sheria mbalimbali za Tanzania. Sura hii inaelezea Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inavyolinda haki za wanawake. Aidha sheria hii pia inaelezea haki na wajibu wa wanandoa.
Aidha sura hii pia inajadili Sheria za Ardhi za Mwaka 1999 zinavyolinda haki za wanawake ikiwamo haki ya kumiliki ardhi, haki sawa katika maamuzi ya ardhi, wajibu wa kupata ridhaa ya mwenzi na wajibu wa kutotumia mila potofu kukandamiza wanawake.

Sura hii pia inaelezea Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004, ambayo imeainisha haki na wajibu wa mfanyakazi pamoja na masuala mengine yahusuyo ajira. Haki ya wafanyakazi wanawake pia imebainisha ikiwamo usawa sehemu za kazi, mapumziko ya uzazi, wajibu wa kuzingatia afya ya mama mjamzito na mtoto. Aidha sura hii ya sita inaelezea Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU na UKIMWI, 2008 inavyomlinda mwanamke ikiwamo majukumu ya kisheria kuhusu UKIMWI.

**Sura ya Saba** inaelezea Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16. ikiainisha makosa mbalimbali ya kujamiiana kama kosa la kubaka, bughudha/shambulio la kijinsia na kadhalika.

**Sura ya Nane** inajadili vyombo vya usimamizi wa haki dhidi ya ukatili wa kijinsia katika ngazi ya kimataifa, ngazi ya kikanda (Afrika), na ngazi ya kitaifa (Tanzania).

**Sura ya Tisa** inajadili jitihada, mafanikio na changamoto mbalimbali dhidi ya ukatili wa kijinsia, zikiwemo jitihada zilizofanywa na AZAKI, zile zilizofanywa na jamii pamoja na zile za mashirika ya maendeleo au wahisani. Sura hii pia imejadili changamoto zinazorudisha nyuma jitihada hizi.

**Sura ya Kumi** na ya mwisho inajadili mapendekezo ya jumla ili kupunguza na hatimaye kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa ujumla. Mapendekezo hayo yanaelekezwa kwa serikali, taasisi mbalimbali, jamii na wadau wa maendeleo kwa ujumla wake.

SURA YA

# 1




# Jinsia na Haki za Binadamu/ Mwanamke

# JINSIA NA HAKI ZA BINADAMU/ MWANAMKE

## 1.1 UTANGULIZI

Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Jinsia wa Tanzania wa 2005, unainisha kuwa suala la jinsia, hususani kutokuwa na usawa, ni kikwazo kikubwa kikuu cha maendeleo ya binadamu na pia ni chanzo kikuu cha ukiukwaji wa haki za binadamu hususan wanawake kama ambavyo imebainishwa hapa chini.

Sehemu hii ya kwanza, inatoa tafsiri ya maana ya jinsia, jinsi na haki za binadamu kwa kuainisha mahusiano ya masuala yote haya. Lengo ni kuleta ufahamu mzuri wa masuala yaliyomo katika sura nyingine za kitabu hiki.

## 1.2 DHANA YA JINSI NA JINSIA

Kumekuwa na mchanganyiko wa uelewa juu ya tofauti katika ya "Jinsi" na "Jinsia." Baadhi ya watu wamekuwa waki-tumia maneno haya kama neno moja. Hata hivyo, maneno haya yana maana tofauti. Sera ya Maendeleo ya Wan-awake na Jinsia ya Mwaka 2000 inatoa tafsiri ya dhana ya maneno hayo.

### *1.2.1 Dhana ya Jinsi*

"Jinsi" ni maumbile ya mwanamke au mwanaume. Ndivyo tulivyo umbwa/kuzaliwa. Majukumu ya wanawake yatokanayo na jinsi zao ni kuzaa na kunyonyesha watoto wakati wanaume wakiwa na majukumu tofauti na hayo. Jinsi ni vile ulivyo mke au mume. Huwezi kubadili. Ndivyo Mungu alivyokuumba.

### *1.2.2 Dhana ya Jinsia*

"Jinsia" ni mahusiano ya kijamii kati ya wanawake na wanaume namna yalivyojengwa na yanavyoendelea kujengwa na jamii kutokana na mila, desturi na tamaduni katika nyanja mbalimbali za umiliki wa mali, mgawanyo wa mapato, fursa za elimu, kurithi mali, kazi/ajira na nafasi mbalimbali za uongozi au ngazi ya maamuzi. Mtazamo huu hutofautiana kati ya jamii au kabila moja hadi nyingine na hubadilika kutokana na wakati.

*Uzoefu unaonyesha kuwa, pamoja na kutambua tofauti zao za kimaumbile, mgawanyo wa majukumu ya kazi, mapato na rasilimali nyingine, fursa za kushiriki katika siasa na utawala, mila na desturi mbalimbali zimekuwa zikiwanyima wanawake nafasi. Hii ni kutokana na mitazamo ya kihistoria ambayo imejikita katika mfumo dume ambao humuona mwanamke kama mtu dhaifu ukilinganisha na mwanaume.*

Mtazamo huu ndiyo hasa sababu ya kutokutoa fursa sawa katika elimu, ajira nzuri, mapato, umiliki mali, uongozi na kadhalika. Bila shaka, uchache wa wanawake katika fani za kitaaluma kama vile udaktari, ualimu, uanasheria, uongozi, urubani na upolisi/ jeshi, unatokana na sababu hizi. Ifahamike kuwa, ukosefu wa usawa kutokana na mi-tazamo hiyo ya kijinsia ni ukiukwaji wa haki za binadamu ambazo, msingi wa usawa, ni moja ya nguzo zake kuu.

## 1.3 JINSIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kwa mujibu wa sheria na mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu haki za binadamu, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya jinsia na haki za binadamu, utu, uzalishaji wa kiuchumi na hata maendeleo ya kisiasa katika jamii yeyote ile Tanzania ikiwemo.

Kwa mfano, ukosefu wa usawa baina ya wanaume na wanawake unaotokana na mitazamo potofu, ni ukiukwaji wa haki ya usawa ambayo ni haki ya msingi kabisa ya kila binadamu. Vilevile, utekelezaji wa baadhi ya mila potofu ambazo huletea ukatili wa kijinsia, ni ukiukwaji wa moja kwa moja wa haki za binadamu.

## 1.4 MAANA YA HAKI ZA BINADAMU

Haki ni dhana inayotokana na hali ya kustahili kitu fulani, yaani mazingira au mahusiano yake na mtu mwingine yanakustahilisha kupata kitu fulani au kutendewa kwa namna fulani na mtu mwingine. Kwa kifupi haki ni stahili ya mtu.

*Hivyo basi, haki za binadamu ni zile stahili ambazo kila mwanadamu anazo au anastahili kuwa nazo kwa kuwa tu, yeye ni binadamu. Stahili hizi ni haki za kuzaliwa za kila mwanadamu, na hivyo, ulinzi wa haki za binadamu ni jukumu la kwanza la kila serikali na jamii nzima.*

Misingi ya haki za binadamu imejengeka katika ukweli kuwa wanadamu wote wanastahili heshima ya kibinadamu, kuwa, binadamu wote wana stahili haki hizo bila kujali jinsia, rangi, utaifa, lugha, umri, hali ya kijamii, dini au msimamo wa kisiasa.

## 1.5 AINA YA HAKI ZA BINADAMU

Haki zinaweza kuchanganuliwa katika makundi matatu, ambayo kwa njia moja ama nyingine, yanaingiliana katika kuelezea/ kulinda haki mbalimbali:

### *1.5.1 Haki za Itikeli*

Hizi ni stahili zinazotokana na kanuni za kiutamaduni, mila au dini. Chini ya mifumo ya kitamaduni, kimila au kidini zipo stahili fulani ambazo watu fulani wanazipata kwa mujibu wa nafasi zao. Mfano haki ya mtu mzima katika jamii fulani fulani kuamkiwa na watu wadogo, haki ya mtoto wa kwanza katika jamii fulani kupewa zawadi fulani na mzazi wake n.k. Haki hizi ni stahili tu za kimazoea na hazina nguvu yoyote kisheria. Haziwezi kufanywa msingi wa madai mahakamani.

### *1.5.2 Haki za Kisheria*

Hizi ni haki ambazo zimeainishwa katika sheria za nchi na hivyo yoyote mwenye kukiukiwa haki hizo anastahili kufungua shauri mahakamani, akidai utekelezaji wake, kulipwa fidia n.k. Haki hizi ni pamoja na haki zote zilizoorodheshwa katika sehemu ya tatu ya sura ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuanzia Ibara ya 12 hadi 29. Haki hizi ni pamoja na haki ya usawa, haki ya kuishi, haki ya uhuru wa binafsi, uhuru wa kuabudu, uhuru wa kukusanyika na kujumuika n.k.

### *1.5.3 Haki za Ki-binadamu*

Hii ni misingi ya jumla ya haki na usawa miongoni mwa wanadamu. Hizi ni haki zilizokubalika kidunia kwamba kila binadamu anazistahili kwa kuwa tu yeye ni binadamu. Haki hizi mara nyingine huitwa haki za asili au haki zilizotolewa na Mungu, kwani hazipokelewi kutoka kwa mtu mwingine wala kununuliwa au kurithiwa bali kila mtu anapozaliwa akiwa binadamu anakuwa nazo bila kujali jinsi, rangi, asili, lugha, taifa, dini, tabaka au msimamo wake kisiasa.

## 1.6 UTAMBUZI NA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU KISHERIA

Pamoja na ukweli kuwa haki za binadamu ni stahili ambazo mtu huzaliwa nazo, kwa utaratibu wa kibinadamu wa utawala wa sheria, unalazimu haki hizo kutambuliwa na sheria husika ili mtu anayekiukiwa stahili yake aweze kuzidai kwa mujibu wa sheria hiyo.

Ni kwa mantiki hiyo basi Umoja wa Mataifa uliamua kuziainisha kwa maandishi kupitia Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la tarehe 10 Disemba, 1948 ili kurahisisha ufuatiliaji wake.

*Tamko hili linajumuisha haki zote za binadamu za aina mbalimbali na kuweka jukumu kwa kila nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa (Tanzania ikiwemo) kuzitekeleza.*

Utekelezaji wa haki zilizobainishwa katika Tamko hili unafanyika kupitia mikataba mbalimbali ya kimataifa pamoja na sheria za kila nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa kama ambavyo imeelezwa kwa kirefu katika kitabu hiki katika sura zinazofuata.

## 1.7 MISINGI YA HAKI ZA BINADAMU KWA MUJIBU WA TAMKO LA 1948

Mbali na kutaja haki mbalimbali, Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948 limeweka pia misingi mikuu saba ya haki za binadamu. Misingi hiyo ni kanuni zinazokubalika kutumika katika tafsiri na utekelezaji wa haki za binadamu wote ikiwa ni pamoja na wanawake.

Kanuni hizi au misingi hii inawezesha kuzielewa vizuri na kuzitekeleza kikamilifu haki za binadamu. Misingi hii ni kama ifuatavyo:

a) **Utu:** Lengo la haki zote za binadamu ni kuhakikisha utu wa binadamu unaheshimika na kuzingatiwa kwa kila jambo linalofanyika kwa mfano; kazi, adhabu (Polisi ama Mahakama) au uamuzi wowote unaochukuliwa dhidi ya binadamu uendane na matakwa ya heshima ya utu wake.

b) **Udunia (Universality):** Haki za binadamu ziheshimiwe sawa katika ulimwengu. Hii ina maana kwamba binadamu wote, wa rangi zote na mahali pote wanazo haki hizo kwa sababu wote ni binadamu.

c) **Usawa (Non–Discriminatory):** Haki za binadamu ziko sawa kwa wote kwa maana hazitakiwi kutolewa kwa ubaguzi wa aina yoyote ile kama vile kutokana na rangi, umbile, jinsi, jinsia, dini, kabila, kipato, n.k.

d) **Kutokunyanyasa (Humiliation):** Pia haki za binadamu zinazuia suala lolote linalohusu unyanyasaji wa kijinsia kwani binadamu wote ni sawa.

e) **Ushirikishwaji (Participatory):** Haki za binadamu zinazingatia suala zima la haki sawa katika ushiriki wa kupanga mipango yote ile ya maendeleo.

f) **Kutegemeana (interdependence):** Haki za binadamu zinahusisha maisha ya kila siku ya binadamu hivyo haki moja inategemea utekelezaji wa haki nyingine. Tunapata huu msingi wa kutegemeana kwa mfano upatikanaji wa haki zote unategemea haki ya kuishi.

g) **Hazigawanyiki (Inviolable):** Huwezi kumpa binadamu haki moja halafu ukamnyima haki zingine lazima zote zikamilike kwani haki za binadamu hazigawanyiki.

## 1.8 UTAMBUZI WA HAKI ZA WANAWAKE

Kutokana na tafsiri tajwa hapo juu, haki za wanawake ni stahili zote ambazo wanawake wanatakiwa kuwa nazo kutokana na wao kuwa ni binadamu na pia kutokana na jinsi yao kama wanawake. Dhana ya jinsia haina nafasi kabisa katika kutambua na kutekeleza haki za wanawake kwa kuwa misingi ya haki za binadamu inatambua kanuni za usawa, ushirikishwaji na kadhalika. Kwa mantiki hii, ukatili wa kijinsia wa namna yeyote ile hauna uhalali wa aina yeyote ile kwa kuwa ni kinyume cha haki za binadamu.

*Ifahamike kuwa, nchini Tanzania mfumo mzima wa sheria na haki za binadamu kwa wanawake na wanaume unaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.*

Katiba hii inaeleza kwamba binadamu wote ni sawa na wanastahili kutambuliwa na kuheshimiwa utu wao. Hivyo ni wazi kwamba watu wote hususan wanawake ambao wamekuwa wakinyanyaswa kutokana na jinsi zao ni ukiukwaji wa katiba ya nchi na misingi ya haki za binadamu tajwa hapo juu.

Kuweka usawa wa kijinsia katika mikataba ya kimataifa, sheria na Katiba ya nchi ni moja kati ya jitihada ambazo serikali ya Tanzania imezifanya ili kulinda haki za pande zote mbili ikiwa ni pamoja na kuwa na uwiano sawa kati ya wanaume na wanawake, na hasa kumkwamua mwanamke kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Hivyo basi inahitajika mikakati madhubuti zaidi kwa lengo la kuondoa masuala ya ukatili wa kijinsia kwani pamoja na kuwepo kwa sheria hizo, ukatili bado umekuwa ni kikwazo katika maendeleo ya wanawake.

SURA YA

2




# Ukatili wa Kijinsia, Aina, Chanzo, Sababu na Matokeo yake

SURA YA

3




# Mahusiano kati ya Ukatili wa Kijinsia, Umaskini, Mila na UKIMWI pamoja na Athari zake

# MAHUSIANO KATI YA UKATILI WA KIJINSIA, UMASKINI, MILA NA UKIMWI PAMOJA NA ATHARI ZAKE

## 3.1 UTANGULIZI

Shirika la Umoja wa Mataiafa la UNIFEM, ambalo hushughulika na haki za wanawake, lilisha baini kuwa, VVU na UKIMWI kwa wanawake, ni suala ambalo liko katika uonekano wa desturi za kijinsia. Vilevile, suala la umaskini ni chanzo na sababu ya UKIMWI na ukatili wa kijinsia. Hivyo basi, ukatili wa kijinsia ni sababu na matokeo ya umaskini na UKIMWI. Hali kadhalika, umaskini na UKIMWI ni sababu na matokeo ya ukatili wa kijinsia kwa sehemu fulani.

## 3.2 MAHUSIANO KATI YA UKIMWI NA UKATILI WA KIJINSIA

Taratibu za kitamaduni zinazoamua na kuweka mitazamo ya kijinsia, kwa njia moja ama nyingine inaathiri hali ya wanawake hususan katika masuala ya VVU/UKIMWI. Hivyo basi, ueneaji wa VVU/UKIMWI hapa Tanzania au sehemu yeyote hasa Afrika, kunahusiana moja kwa moja na masuala ya jinsia.

*Vilevile, masuala ya jinsia na ueneaji wa VVU/ UKIMWI unaonyesha kuwa, ijapokuwa ueneaji wa VVU/UKIMWI unapungua Tanzania (kwa mtazamo wa ujumla wa nchi nzima) kwa wanaume na wanawake kiujumla, maambukizo ya VVU/UKIMWI miongoni au kwa wanawake ni ya juu zaidi kuliko wanaume.*

Mfano, takwimu zinaonyesha kuwa, kwa sasa, kiwango cha maambukizi kwa wanawake cha VVU/UKIMWI ni takribani 6.8% ukilinganisha na wanaume ambao kiwango chao cha maambukizi ya ugonjwa huu ni takribani 4.7% pekee. Vile vile, wanawake wanachukua zaidi ya 61% ya watu wote walioambukizwa UKIMWI hapa Tanzania kwa mujibu wa Takwimu za mwaka 2008/2009.

Hivyo basi, wanawake ni wepesi sana wa kuathirika/kuambukizwa na VVU/UKIMWI kuliko wanaume. Hii inatokana na masuala ya kijinsia ilivyosemwa hapo juu, ambayo hasa yanajikita katika mitazamo ya mila na desturi.

## 3.3 SABABU KUU ZA MASUALA YA JINSIA NA UKIMWI

Sababu kuu za masuala ya kijinsia na VVU/UKIMWI zinaweza kuwa ni pamoja na:-

a) Muingiliano wa kingono unaotokana na 'ibada' ama matambiko ya kimila hasa pale ambapo Mume anafariki. Makabila mengi hufanya tambiko la 'Kutakasa Mjane' kwa kumlazimisha kufanya mapenzi na mmoja wa kaka wa marehemu mume wake ili 'kumuondolea mikosi.' Hvyo, kama ndugu huyo ni mgojwa, ni wazi atamuambukiza mjane.

b) Matambiko na imani za kimila kama vile Ukeketaji wa wanawake, ambao, mbali na kuwa ni kitendo cha kutweza, pia mara nyingi hufanywa kwa kutumia vifaa visivyokuwa salama kiafya. Hivyo, kama mmoja ya watu waliokeketwa ni mgonjwa, wengine pia wanaweza kuambukizwa magojwa.

c) Ndoa za wake wengi, ambapo, mmoja tu akiwa ni Mgonjwa, wengine pia huathiriwa.

d) Ndoa za utotoni za kimila ambazo msichana mdogo anakuwa hana uwezo kumtathimini na wa kumkataa mwanaume (aliyechaguliwa) hata kama mwanaume huyo ni mgojwa.

e) Kutokuwa na usawa wa maamuzi kati ya wanaume na wanawake kaika jamii zetu kama tulivyoona katika Mada ya Kwanza, hali ambayo inawafanya wanawake washidwe kuamua juu ya ngono salama.

f) Ubakaji ndani ya ndoa, kwa maana kwamba, wakati mwingine mwanandoa mmoja anagundua kuwa mwenzake ni muathirika wa VVU/UKIMWI, lakini akikataa kufanya naye tendo la ndoa hulazimishwa kwa nguvu pasipo ridhaa yake kisa tu 'tendo la ndoa ni haki ya mwanandoa, Sheria za Tanzania haziko wazi juu ya hili.

## 3.4 MAHUSIANO KATI YA UMASKINI NA UKATILI WA KIJINSIA

Uhusiano wa Jinsia na Umasikini umetajwa katika Sera ya Taifa ya UKIMWI ya 2001 na sera/ mikakati mingine kama ilivyoelezewa hapo awali.

Mkakati wa Kitaifa wa awamu ya pili wa Kupambana na Umasikini wa Tanzania (MKUKUTA II) unabainisha kuwa, ubaguzi wa kijinsia unawapendelea zaidi wanaume. Kwa mfano, kuhusu umiliki ardhi na mali nyingine, au haki ya msichana kupata elimu, vinaongeza machungu ya umasikini kwa kupunguza kipato cha sasa ama kipato tarajiwa cha wanawake. Kwa mantiki hii, kuondosha ubaguzi huu ni changamoto kubwa na muhimu sana.

*Vilevile, Ibara ya 11 ya Tamko la Kimataifa la Uwajibikaji katika VVU/UKIMWI la mwaka 2001 la Umoja wa Mataifa, linasema kuwa, UKIMWI, Umasikini na Ujinga ni masuala yanayotegemeana sana. Hili pia linaungwa mkono na Aya ya 1.6(q) ya Sera ya Taifa ya UKIMWI ya 2001.*

Hivyo utaona kuwa, masuala ya kijinsia, ambayo yanamnyima mwanamke haki ya kumiliki mali, kusoma, kufanya kazi, na kadhalika, yanamfanya awe masikini na tegemezi kwa mume wake ama ndugu wengine wa kiume. Utegemezi wa namna hii husababisha ukatili wa kijinsia kwa sababu wanaume hufanya 'lolote wanalotaka' kwa sababu ndiyo wenye maamuzi ya mwisho.

## 3.5 ATHARI ZA UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili wa kijinsia una athari mbalimbali . Baadhi ya athari hizo ni pamoja na:-

a) **Kisaikolojia:** Ukatili wa kijinsia unaweza kusababisha mtu kuathirika kisaikolojia na hivyo kupelekea, kutojiamini, kujisikia mnyonge wakati wote, kujitenga, kuwa na msongo wa mawazo, kujichukia, kusononeka na hata kufanya mambo ya aibu ambayo mtu wa kawaida asingeliweza kuyafanya.

b) **Kimwili:** Ukatili wa kijinsia unaweza kusababisha mtu kuathirika kimwili na hivyo kupelekea maumivu ya mwili, ukosefu wa viungo vya mwili, ulemavu, kifo, kujifungua kwa taabu, kushindwa kuona na kushindwa kusikia.

c) **Kiuchumi:** Ukatili wa kijinsia unaweza kusababisha mtu kuathirika kiuchumi na hivyo kumfanya awe katika hali ya umasikini uliokithiri, utegemezi, kupoteza rasilimali, kupoteza ajira na kudhalilika kiutu, kwa mfano kufanyishwa biashara ya ngono.

d) **Kingono:** Hali kadhalika ukatili wa kingono unaweza kupelekea athari zifuatazo; kuenea kwa UKIMWI na magonjwa ya zinaa kama, kaswende, kisonono na mengine, kukithiri kwa watoto wa mitaani, kukosa elimu bora, kupata mimba zisizotarajiwa, kutoa mimba, kutokea vifo na kupatikana kwa watoto ambao hawajui baba zao.

SURA YA

# 4




# Ulinzi wa Haki za Wanawake kwa Mujibu wa Mikataba ya Kimataifa

# ULINZI WA HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA MIKATABA YA KIMATAIFA

## 4.1 UTANGULIZI

Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali kuhusiana na ukatili wa kijinsia. Baadhi ya mikataba ya kimataifa ni kama vile Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948; Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa 1979; Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika (Maputo Protocol) wa Mwaka 2003; na Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la 1995.

## 4.2 TAMKO LA KIMATAIFA LA HAKI ZA BINADAMU LA 1948

Kama ilivyoainishwa katika sura zilizopita, usimamizi na utekelezaji wa haki na wajibu wa sasa wa haki za binadamu vina misingi yake katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948.

Tamko hili, kwa sehemu kubwa lilitokana na matokeo mabaya ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1939-1945) ambayo iliambatana na ukiukwaji mkubwa sana wa haki za binadamu. Hali hii ililazimu nchi nyingi duniani kudai kuwepo kwa viwango vitakavyoongoza vitendo vya serikali kwa wananchi wake.

Kati ya haki zilizobainishwa katika Tamko hili ni pamoja na haki ya usawa, uhuru dhidi ya ubaguzi, kuishi, uhuru na usalama wa mtu, uhuru dhidi ya utumwa, mateso au vitendo vya udhalilishaji, kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria, kupata msaada wa mahakama, na uhuru wa kujieleza na kushiriki katika siasa.

*Ili kuweka mazingira mazuri ya ulinzi wa haki zilizomo katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948, Umoja wa Mataifa umepitisha MIKATABA (yaani sheria za kimataifa) mbalimbali. Mikataba hii ina lengo la kuhakikisha utekelezaji wa haki za makundi mbalimbali kama watoto, wanawake, wakimbizi, na kadhalika. Vilevile, Mikataba hii ina lengo la kusimamia haki za aina mbalimbali kama za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni.*

Baadhi ya mikataba iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa ili kutekeleza masharti ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948 ni:-

a) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa 1966;
b) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa 1966.

Baada ya Mikataba hii, kumekuwa na Mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa 1979; Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika (Maputo Protocol) wa Mwaka 2003 na Maazimio ya Kimataiafa ya aina mbalimbali likiwemo Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la 1995.

## 4.3 MKATABA WA KIMATAIFA WA KUONDOA AINA ZOTE UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE (CEDAW) WA 1979

Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa 1979, uliazimiwa na Umoja wa Mataifa tarehe 18 Desemba Mwaka 1979. Tanzania ni sehemu ua utekelezaji wa matakwa ya mkataba huu kwa sababu ilishauridhia mwaka 1985.

Mkataba huu umejikita katika kuelezea vikwazo mbalimbali dhidi ya wanawake kwa kutoa mwongozo kuhusu haki sawa kwa wanawake katika nyanja za kisiasa, kijamii, fursa sawa kielimu pamoja na uwepo wa mitaala ya elimu sawa, kuondolewa kwa ubaguzi katika ajira, malipo, pamoja na uhakika wa kuendelea na kazi katika hali ya ndoa na uzazi.

*Baadhi ya Haki zilizotajwa katika mkataba huu, na kuagiza nchi husika kuhakikisha kuwa hakuna ubaguzi dhidi ya wanawake ni Haki ya Kupiga Kura (Ibara ya 7); Utaifa (Ibara 9); Elimu (Ibara ya 10); Ajira (Ibara ya 11); Afya (Ibara ya 12); Uchumi (Ibara ya 13); na Ndoa (Ibara ya 16).*

Aidha, mkataba huu umetilia mkazo uwepo wa sheria za kitaifa za kupambana na ubaguzi dhidi ya wanawake na kupendekeza hatua za muda zitakazochukuliwa ili kuharakisha kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake katika mambo ya kijamii na kimila ambayo hufuga na kulea ubaguzi.

Kuhusu masuala ya kijamii, mkataba huu unatilia mkazo huduma za kijamii hususan mahitaji na utunzaji wa watoto na wajibu wa familia, madaraka ya kikazi na maisha ya kijamii. Vifungu vya ziada vya mkataba huu vinatilia mkazo wa kuondokana na ubaguzi dhidi ya wanawake hasahasa katika huduma za afya na uzazi. Aidha, msisitizo umewekwa kwenye uwezo sawa wa kisheria kwa wanaume na wanawake. Matatizo ya wanawake vijijini pia

yamepewa kipaumbele zaidi.

Mkataba huu pia umeweka taratibu za usimamizi wa kimataifa juu ya wajibu wa nchi wanachama kama zilivyokubalika na mataifa mbalimbali.

## 4.4 MKATABA WA NYONGEZA WA HAKI ZA WANAWAKE BARANI AFRIKA (MAPUTO PROTOCOL) WA MWAKA 2003

Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika wa Mwaka 2003 ni Mkataba wa nyongeza kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.

Mkataba huu ilitiwa saini na nchi za umoja wa Afrika Jijini Maputo, Msumbiji tarehe 11 Julai mwaka 2003. Jina la "Maputo Protocol" linatokana na sababu hiyo.

Tanzania iliridhia Mkataba huu mnamo tarehe 3/3/2007 na kukubali kama nchi kubanwa na masharti yaliyomo. Hata hivyo, kama ilivyo katika utekelezaji wa mikataba mingine, kwa mfumo wa sheria wa Tanzania, mkataba huu hauwezi kumwajibisha mwananchi moja kwa moja au mtu kuutumia pale ambapo anaona umekiukwa.

*Ifahamike kuwa, kuazimiwa na kusainiwa kwa Mkataba huu ilikuwa ni matokeo ya ushawishi wa shirika la WiLDAF ambao walitoa wazo la kuwepo Mkataba wa namna hii ili kuziainisha haki za mwanamke katika muktadha wa hali ya kiafrika badala ya kidunia nzima kama zilivyo-ainishwa na mkataba wa CEDAW.*

Nchi yetu inafuata msingi kuwa sheria za Kimataifa ni tofauti na sheria za Kitaifa. Kwa hiyo, kama yanavyojieleza kwenye Ibara ya 2 ya Mkataba huu, Tanzania inapaswa kuuingiza mkataba huu katika sheria za nchi kwa kufanya yafuatayo:-

a) Kuingiza katika katiba za nchi na sheria zinginezo, kama bado hazijafanya hivyo, kanuni ya usawa kati ya wanawake na wanaume na kuhakikisha zinatimizwa;
b) Kutunga na kutekeleza sheria mahsusi na kuweka mwongozo ikiwemo ile inayopinga na kukataza kabisa aina zote za ubaguzi hususani matendo yenye madhara kwa wanawake ambayo yanahatarisha afya na ustawi wa wanawake kwa ujumla;
c) Kufuata mtazamo wa kijinsia katika maamuzi ya sera, sheria, mipango ya maendeleo na shughuli zote katika upana wote wa maisha;
d) Kuchukua hatua za kusahihisha na za makusudi katika maeneo ambayo ubaguzi wa kijinsia bado unaendelea;
e) Kuunga mkono harakati za kuondoa ubaguzi kimataifa, kikanda na kitaifa.

## 4.5 HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA MKATABA WA MAPUTO PROTOCOL

### *4.5.1 Mirathi na Haki za Wajane*

Tunafahamu kuwa Sheria za sasa za Tanzania za Mirathi kwa kiasi kikubwa zinanyanyasa wajane na watoto wa kike, kwa mfano, Sheria za kimila haimtambui mjane kama mrithi, bali hurithi kupitia watoto wake. Aidha, Kanuni za sheria hii zinamchukulia mtoto wa kike kama mtu wa daraja la tatu baada ya mtoto wa kiume (daraja la 1), watoto wengine wa kiume (daraja la 2).

Mkataba wa Maputo unakomesha uonevu huu na kueleza kuwa endapo mume atafariki, basi mke atakuwa mrithi moja kwa moja wa mali na mlezi wa watoto. Kwa mfano, Ibara za 20 na 21 za Mkataba huu zinabainisha kuwa, mjane au mwanamke yeyote ana haki ya:-

a) Kutokuwekwa katika hali ya unyanyasaji, udhalilishaji na matendo ya kushushiwa hadhi;
b) Kuwa mlezi wa moja kwa moja wa watoto wake ispokuwa tu kama ni kinyume na maslahi/ustawi wa mtoto;
c) Kuoelewa tena akipenda na kwa ridhaa yake;
d) Kurithi mali ya mume wake, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuishi katika nyumba ya ndoa; na
e) Kurithi katika mafungu linganifu kutoka kwa mali za wazazi wao.

### *4.5.2 Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake*

Mkataba wa Maputo unaitaka Serikali kuhakikisha inatunga sheria mpya ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake. Ibara ya 3 ya Mkataba huu inakataza kabisa Ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake na kuitaka nchi itunge sera, sheria na miongozo ya kupinga ukatili huo.

Ibara za 5 na 8 za Mkataba huu zimeelekeza kuwa wahanga wa ukatili wa kijinsia wapate msaada wa kisheria na pia matibabu ya kisaikolojia na masomo ya ufundi ili warudi katika hali ya kawaida ya awali.

*Mara nyingi msaada wa kisheria hutolewa na asasi za kiraia tu, ni wakati sasa serikali iweke bajeti ya msaada wa kisheria na ujenzi wa nyumba za matumaini kwa walioathirika na ukatili wa kijinsia wakati wakisubiri kupeleka mashauri yao mahakamani.*

*4.5.3 Wanawake katika Ngazi za Maamuzi*

Wanawake katika ngazi za maamuzi imeongelewa kwa upana sana katika Mkataba huu. Ibara ya 9 ya Mkataba inaeleza kuwa, katika ngazi zote za maamuzi wanawake na wanaume wawakilishwe sawa lakini pia kuwe na jitihada za makusudi za kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi, ukizingatia kuwa wanawake walikuwa wamebanwa na mila na desturi potofu hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu katika vyombo vya utoaji maamuzi.

*4.5.4 Mila Potofu na Matendo yenye Madhara*

Ibara ya 5 ya Mkataba huu inakataza kabisa matendo yenye madhara kwa mfano ukeketaji kwa marika yote. Hapa Tanzania Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kifungu cha 169A kinakataza ukeketaji kwa watoto pekee (chini ya miaka 18). Hata hivyo, taarifa mbalimbali za kitafiti ambazo zimekuwa zikitolewa zinaonyesha kuwa, wakati mwingine wanawake watu wazima wamekuwa wakikeketwa wakati wa kujifungua pale wanapoolewa kwenye jamii zinazokeketa. Aidha, jamii hizi pia zimeanzisha utaratibu wa kukeketa watoto wachanga.

Mauaji ya wanawake vikongwe kwa imani za kishirikina inakatazwa katika Ibara ya 22 ya Mkataba huu. Ibara ya 6 inakataza ndoa za utotoni. Kurithi wajane pia ni vitendo vinavyokatazwa kwenye vifungu vingine vya Mkataba huu. Ibara ya 14 inatambua kuwa UKIMWI ni suala mtambuka ambapo, waathirika wakubwa wa maambukizi ni wanawake kwa kuugua na pia kulea wagonjwa majumbani bila malipo, elimu ya kutosha juu ya VVU/UKIMWI na vifaa husika.

## 4.6 AZIMIO LA BEIJING LA MASUALA YA JINSIA LA 1995

Mkutano wa Beijing uliofanyika mwaka 1995, katika jiji la Beijing, China, ulibainisha maeneo ya kipaumbele kwa serikali zetu. Maeneo hayo ni pamoja na:-

a) Kuwapatia wanawake haki na kuwaongezea uwezo kisheria;
b) Kuwawezesha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi;
c) Kuimarishia wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini; na
d) Kuwapatia wanawake elimu, mafunzo na ajira.

Pamoja na mambo yake mazuri, Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la mwaka 1995 bado linahitaji kuwafikia wanawake walio wengi zaidi.

SURA YA

5




# Ulinzi wa Haki za Wanawake kwa Mujibu wa Katiba ya Tanzania

# ULINZI WA HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA KATIBA YA TANZANIA

## 5.1 UTANGULIZI

Nchi yoyote ambayo inafuata misingi ya demokrasia, utawala bora, haki za binadamu na kuzingatia utawala wa sheria inaongozwa na Katiba ambayo ni sheria mama ya nchi husika. Tanzania inaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katiba hii ndiyo inayoweka kanuni za jumla za utungaji wa sheria za nchi.

Kwa mujibu wa Ibara ya 64(5) ya Katiba hii, sheria yoyote itakayotungwa kwa kukinzana na Katiba inakuwa batili. Makahama ina uwezo wa kutamka kuwa sheria hiyo ni batili.

## 5.2 HAKI NA WAJIBU MBALIMBALI KWA MUJIBU WA KATIBA YA TANZANIA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 imeweka Ibara mbalimbali zinaota wajibu na kulinda haki na usawa wa mwanamke kama ifuatavyo:-

### *5.2.1 Fursa Sawa ya Elimu na Mafunzo*

Kwa kuzingatia usawa wa binadamu, Katiba katika Ibara ya 11 (3) imetamka bayana kuwa kila mtu ana haki ya kupata fursa sawa za elimu na mafunzo bila kujali jinsi. Hii inamaanisha kwamba wanawake wana haki sawa na wanaume ya kupata fursa mbalimbali za elimu na kujiendeleza kimasomo.

### *5.2.2 Ulinzi wa Utu wa Mtu*

Ibara ya 12(2) imeweka bayana haki ya kila mtu kupata ulinzi na kuheshimiwa utu wake. Hivyo basi vitendo vyovyote pamoja na kauli zinazopelekea kudhalilisha utu na heshima za wanawake vinakiuka misingi ya Katiba.

### *5.2.3 Usawa Mbele ya Sheria*

Kwa mujibu wa Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Tanzania, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa. Kwa tafsiri ya Ibara hii, wanawake wana haki sawa kama ilivyo kwa wanaume. Hivyo vitendo vyovyote vinavyozuia upatikanaji wa haki kwa wanawake mbele ya sheria vinakiuka Ibara hii.

*Migogoro kuishia katika ngazi ya familia ni jambo jema. Hata hivyo mara nyingi wanawake wamekuwa wakikandamizwa na maamuzi ya familia na kunyimwa haki zao kutokana na mila na desturi nyingi ambazo hazitoi fursa sawa baina ya wanaume na wanawake katika kuzungumza au kujitetea kutokana na mgogoro uliopo. Hivyo basi familia zimekuwa zikishindwa kutoa maamuzi sahihi na ya haki kutokana na uwiano wa mgogoro uliopo. Hii hupelekea mgogoro au tatizo kuendelea na kuleta madhara na maafa makubwa katika familia.*

Ibara ya 13 (3) inatoa ulinzi wa haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu kulindwa na kuamuliwa na Mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka ya nchi vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia vinavyodhuru afya na mali za wahanga wa ukatili havina budi kushughulikiwa na vyombo vya sheria.

### *5.2.4 Ulinzi Dhidi ya Ubaguzi na Mateso ya Aina Zote*

Ibara ya 13(5) ya Katiba ya Tanzania, inakataza ubaguzi wa aina yoyote ile ikiwemo ubaguzi wa kijinsia. Hivyo wanawake hawatakiwi kubaguliwa kutokana na jinsi zao.

Ibara ya 13(6)(e) ya Katiba hii inakataza mtu yeyote kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha. Kwa namna hiyo, mtu yeyote anayefanya vitendo vya ukatili wa namna hii, anavunja sheria.

*5.2.5 Haki ya Kuishi*

Ibara ya 14 ya Katiba ya Tanzania, inahakikishia haki ya kuishi kwa kila mtu. Mantiki ya Ibara hii inaweza kuwa ukatili wa kijinsia una athari kubwa kwa binadamu, mathalani unaweza kupelekea kifo kwa wahanga wa ukatili kutokana na madhara au majeraha waliyopata. Ni haki kwa kila mtu kuishi katika hali ya usalama na kusaidiwa pale itakapobidi kutimiza haki hii ya kuishi.

*Imekuwa ni jambo la kawaida kwa watu binafsi, vyombo vya dola na kadhalika kushindwa kuwahifadhi wahanga wa ukatili wa kijinsia pale wanapohitaji msaada huo. Sababu kubwa imekuwa ni kutokuwa tayari "kuingilia migogoro inayohusu mahusiano ya wanafamilia." Kwa kufanya hivi, ni kukiuka ibara ya 14 ya katiba inayotamka bayana kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.*

*5.2.6 Haki ya Kuishi Kama Mtu Huru*

Ibara ya 15 ya Katiba inatambua kuwa watu wote wako huru. Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

Ibara ya 15(2) inakataza mtu yeyote kufanya hivyo, yaani ni marufuku mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake.

*Imekuwa ni jambo la kawaida katika jamii zetu kukandamiza na kuinyima uhuru jinsi ya kike. Katika baadhi ya makabila hapa nchini kumekuwa na desturi za kukamata wanawake kwa nguvu na kuwafungia kwa lengo la kuanzisha mahusiano ya mke na mume.*

*5.2.7 Haki ya Faragha na Usalama wa Mtu*

Ibara ya 16(1) ya Katiba ya Tanzania inatamka bayana kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi.

*5.2.8 Uhuru wa mtu kuenda atakako katika jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Ibara ya 17(1) ya Katiba ya Tanzania inasema, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na Kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.

Kifungu hiki kinampa haki mwanamke kama raia mwingine yeyote kwenda mahali popote anapotaka kwa maslahi yake binafsi, ya familia au ya taifa.

*Kulingana na takwimu za utafiti iliyofanywa na idara ya takwimu ya mwaka 2010 inayoonyesha kwamba asilimia 37 ya wanawake waliohojiwa wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mkewe kwa sababu ya kuondoka nyumbani bila kumuaga mumewe. Hii ni ukiukwaji wa Katiba.*

*5.2.9 Uhuru wa Maoni na Kupata Habari*

Ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania, inatamka kuwa kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni na fikra zake bila kubughudhiwa. Vilevile, kila mtu anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi. Ibara ya 18(c) inatoa haki ya kufanya mawasiliano na haki ya kutokuingiliwa katika mawasiliano.

Huu ni ukatili mkubwa wa kijinsia na ukiukwaji wa Katiba ya nchi. Hali hii humfanya mwanamke akose taarifa muhimu hata za kuhusu masuala ya afya na uzazi kwa ujumla. Hali hii huwaweka wanawake katika mazingira hatarishi na uwepesi wa kunyanyasika kila wakati ukilinganisha na wanaume.

*Imekuwa ni jambo la kawaida katika jamii zetu hapa nchini ambapo wanawake walio wengi hawahusishwi katika kupata habari, kuchangia au kutoa maoni yao binafsi pale inapobidi. Hali kadhalika mila nyingi zinatoa kipaumbele kwa watu wa jinsi ya kiume kuwa ndio wenye sauti na maamuzi ya mwisho katika ngazi za familia na kiutawala.*

*5.2.10 Uhuru wa Mtu Kushirikiana na Wengine*

Ibara ya 20 ya Katiba hii pia imeweka uhuru kwa mtu yeyote kushirikiana na wengine kwa hiari yake na watu wengine ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika kwa madhumuni ya hifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake. Mijumuiko inaweza kuwa ni vikundi vya akina mama au vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS). Hivyo, kisheria na kikatiba ni marufuku kumzuia mtu yeyote kushirikiana na mwingine/ wengine.

*5.2.11 Haki ya Kufanya Kazi na Kupata Ujira wa Haki*

Ibara ya 22 na 23 za Katiba ya Tanzania zinatamka kuwa, kila mtu anastahili fursa sawa, kwa masharti ya usawa, ya kushiriki nafasi yeyote ya kazi na shughuli yeyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi. Vilevile, kila mtu anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na malipo ya haki.

*Kuna jamii ambazo zinanyima fursa ya kufanya kazi kwa wanandoa hususan kwa upande wa jinsi ya kike. Katika baadhi ya makabila wanawake hawapewi nafasi ya kazi yenye tija kama ilivyo kwa wanaume kwa mfano kuuza duka, kusimamia shughuli ya mashine n.k. Utakuta mwanaume au ndugu wa mume hutaka mke abaki kulinda nyumba na kufanya kazi za nyumbani na hivyo kuwazuia wanawake kutoka nyumbani. Vitendo hivyo ni kinyume cha Katiba na sheria za nchi.*

*5.2.12 Haki ya Kumiliki Mali*

Ibara ya 24 ya Katiba ya Tanzania inatoa mwongozo kwamba kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya kuhifadhi mali aliyonayo bila kuathiri masharti ya sheria za nchi.

Hivyo kuwanyima haki ya kumiliki na kuhifadhi mali ambazo wana maslahi ya moja kwa moja ni kuvunja haki zao za kikatiba kwa mujibu wa Ibara hii.

*Mara nyingi tumeshuhudia wanawake na watoto wakinyang`anywa mali zao pale wanapofiwa na waume ama wazazi kwa upande wa watoto kwa sababu tu baadhi ya mila na desturi haziwapi nafasi ya wao kumiliki mali za marehemu pamoja na wao kuwa wahusika wakuu kwenye mali hizo.*

SURA YA

6




# Ulinzi wa Haki za Wanawake kwa Mujibu wa Sheria Mbalimbali za Tanzania

# ULINZI WA HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA SHERIA MBALIMBALI ZA TANZANIA

## 6.1 UTANGULIZI

Mbali na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 iliyozungumziwa katika sura iliyopita, kuna sheria mbalimbali zinazowalinda wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia. Baadhi ya sheria hizo ni pamoja Sheria ya Ndoa 1971, Sheria za Ardhi 1999, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini 2004, Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Watu ya mwaka 2008; na Sheria ya VVU na UKIMWI ya 2008.

## 6.2 SHERIA YA NDOA YA MWAKA 1971

Sheria hii ndiyo inayosimamia taratibu za aina zote za ndoa hapa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya haki na wajibu kwa watu walio katika ndoa katika masuala ya matunzo ya watoto, mali za familia na talaka. Kwa mujibu wa Sheria hii ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote.

## 6.3 AINA ZA NDOA KWA MUJIBU WA SHERIA

Sheria hii imeainisha aina mbili za ndoa:-

*6.3.1 Ndoa ya Mke Mmoja*

Sheria hii inatoa msisitizo kwamba ndoa kati ya Wakristo iliyofungwa Kanisani, haiwezi kugeuzwa kuwa ndoa ya mitala, kwa maana ya ndoa zaidi ya mke mmoja endapo wanandoa hao wataamua kubakia katika ukristo. Mwanaume aliyeoa kwa ndoa ya mke mmoja hataruhusiwa kufunga ndoa nyingine isipokuwa tu pale anapofiwa na mke wake.

*6.3.2 Ndoa ya Wake Wengi/ Ndoa za Mitala*

Ndoa hizi zina weza kuwa za Kiislamu au Kimila, zinatambuliwa na sheria hii. Ndoa yenye madhumuni ya kuwa na mke zaidi ya mmoja haitaweza kugeuzwa kuwa ya mke mmoja. Kwa maana hiyo mwanaume aliyeoa kwa ndoa ya wake wengi hawezi kufunga ndoa na mke mwingine kwa taratibu zile zinazotumika katika ndoa ya mke mmoja.

*6.3.3 Taratibu mbalimbali zinazotumika katika kufunga Ndoa*

Sheria ya ndoa inatambua taratibu mbalimbali za kufunga ndoa ikiwa ni pamoja na:-

a) **Kimila:** Utaratibu huu unatumiwa na sheria ya kimila ambapo jamii na makabila mbalimbali hutumia taratibu hizi. Hata hivyo utaratibu huu unapungua kutokana na mwingiliano wa kuoana watu wa makabila tofauti tofauti.

b) **Kidini:** Huu ni utaratibu ambapo ndoa inafungwa kwa taratibu za kidini. Inaweza kuwa kwa utaratibu wa dini ya Kiislamu, Kikristo ama dini zingine.

c) **Kiserikali:** Utaratibu huu ni ule ambao ndoa inafungwa mbele ya Afisa wa Serikali mwenye mamlaka ya kufungisha ndoa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

d) **Dhania:** Huu ni utaratibu wa dhana ya ndoa ambapo sheria inatambua kwamba endapo itathibitishwa kwamba mwanaume na mwanamke wenye sifa za kufunga ndoa, wameishi mfululizo kwa miaka miwili au zaidi chini ya paa moja na wakapata heshima ya mke na mume, basi watachukuliwa kuwa mke na mume hata kama hawajapata mtoto.

*Sifa za Wanandoa*

*a) Wanandoa ni lazima wawe na jinsi tofauti.*
*b) Wanandoa hawapaswi kuwa ndugu.*
*c) Kusiwepo na pingamizi lolote.*
*d) Kwa upande wa Kiislamu mke asiwe katika kipindi cha eda (yaani miezi mitatu toka alipoachwa au miezi minne na siku kumi toka alipofiwa na mume).*

## 6.4 BAADHI YA HAKI ZA MWANAMKE KWA MUJIBU WA SHERIA YA NDOA

Sheria ya Ndoa ya 1971 ina vifungu mbalimbali vinavyoweza kumlinda mwanamke dhidi ya ukatili wa kijinsia. Baadhi ya vifungu hivyo ni: -

### *6.4.1 Haki ya Kutoshurutishwa Kuingia Katika Ndoa*

Kifungu cha 16 cha Sheria hii kinampa nafasi mwanamke haki ya kuingia kwenye ndoa pasipo kulazimishwa na mtu yeyote. Hata hivyo imekuwa kawaida kwa jamii na makabila mbalimbali kukiuka haki ya wanandoa kuingia kwenye ndoa kwa hiari kwa sababu ya mila na desturi zinazowazunguka. Sababu nyingine ni ya umasikini unaoweza kuwalazimsha watu kuingia katika ndoa pasipo wao kuridhia. Hii ni kinyume cha sheria hii.

### *6.4.2 Haki ya Kupinga Ndoa Nyingine*

Kifungu cha 20 cha Sheria hii kinampa nafasi mwanamke aliyeolewa kupinga ama kuzuia endapo mume anataka kuongeza mke mwingine kinyume na taratibu za ndoa iliyofungwa. Kwa mantiki hiyo, sheria hii iko wazi kwa ajili ya kuheshimu mkataba wa mwanandoa ili kulinda heshima kwa wanawake wasiwe sehemu ya kuchezewa na waume zao kwa kuoa kila mwanamke wanayemtaka.

### *6.4.3 Haki ya Kumiliki na Kutumia Mali*

Vifungu vya 56 na 58 vya Sheria hii vinampa haki mwanamke haki ya kumiliki, kutumia na kuuza mali yake mwenyewe inayohamishika na isiyohamishika kama ilivyo kwa mwanaume.

*Hata hivyo kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya sheria kwa wanawake na wanaume, wanawake wengi hawaipati haki hii kwa kuwa mambo mengi yanafanywa kwa mazoea kwamba mwanaume ndio kila kitu na kwamba mwanamke ndani ya ndoa anapaswa kupewa maelekezo na mume ambapo yeye anakuwa ni mtekelezaji tu.*

### *6.4.4 Wajibu wa Kuomba Ridhaa ya Mwanandoa*

Kifungu cha 59 cha Sheria ya Ndoa ya 1971 kinamkataza mmoja wa wanandoa kuuza, kugawa, kukodisha ama vinginevyo mali ambayo ni ya wanandoa pasipo idhini ya mwanandoa mwingine. Kifungu hiki kinaweza kumlinda zaidi mwanamke kama yalivyo tolewa maelezo ya awali kuwa umiliki na maamuzi mengi ndani ya nyumba ya wanandoa hufanywa na wanaume pasipo kushirikisha wake zao tangu awali.

### *6.4.5 Haki na Wajibu wa Kupata Matunzo*

Kifungu cha 63 cha Sheria hii kinaelezea bayana wajibu wa kumtunza mwenzi hadi hapo wanandoa watakapokuwa wametengana kwa makubaliano au kwa amri ya Mahakama na kulingana na amri iliyopo ya Mahakama.

a) Ni wajibu wa kila mwanamume kumtunza mkewe au wake zake na kuwapa malazi, mavazi na chakula kadri ya uwezo na nafasi yake katika maisha.

b) Ni wajibu wa kila mke ambaye ana uwezo wa kufanya hivyo, kumhudumia mume wake kama hana uwezo, (kitimilifu au kwa kiasi fulani) kutokana na kuumia kiakili au kimwili au afya mbaya (ugonjwa).

### *6.4.6 Haki ya Kukopa kwa Jina la Mume*

Kifungu cha 64 cha Sheria hii kinatoa nafasi kwa mwanamke kuomba mkopo kwa jina la mume wake au kwa ajili ya kujikimu. Kulingana na vifungu vidogo namba (2) na (3), mwanamke anadhaniwa, hadi ikithibitika vinginevyo, kuwa na mamlaka ya kuomba mkopo kwa jina la mumewe, au kukopa fedha kwa jina la mumewe au kutumia sehemu ya pesa iliyoko mkononi mwa mumewe au chini ya uthibiti wa mumewe, au kuuza mali ya mumewe.

### *6.4.7 Haki ya Kutoadhibiwa/ Kuteswa*

Kifungu cha 66 cha Sheria ya Ndoa ya 1971 kinaeleza kwamba pasipo kujali mila yoyote, hakuna mtu mwenye haki ya kumpa adhabu inayomdhuru mwanandoa mwingine.

Hivyo sheria hii iko wazi kwamba mwanandoa hawezi kumpiga mwanandoa mwingine kwa visingizio vya kuwepo kwa mila, desturi na mazoea ya jamii fulani.

*6.4.8 Haki ya Mjane Kufanya Maamuzi Apendavyo*

Kifungu cha 68 cha Sheria hii kinampa mjane haki na uhuru wa kuishi anapotaka yeye na hata kutoolewa au kuolewa tena na mwanaume amtakaye bila kubanwa na taratibu zozote za kimila, isipokuwa kwa mwanamke mjane aliyekuwa amefunga ndoa ya Kiislamu hatatakiwa kuolewa na mtu mwingine mpaka kitakapomalizika kipindi cha eda.

*Kifungu hiki kinaziba mianya inayotumika kimila kwamba mjane anatakiwa kurithiwa na wanaukoo au kwamba mjane haruhusiwi kuolewa na kuishi katika nyumba aliyokuwa anaishi na mume wake ambaye ni marehemu.*

*6.4.9 Haki ya Kutengana*

Kifungu cha 99 cha Sheria hii kinatoa nafasi kwa wanandoa kuomba kutengana kwa muda au moja kwa moja ikiwa kuna sababu maalumu.

*Kifungu hiki kilitungwa maalumu kwa ajili ya kuwasaidia wanandoa hasa upande wa wanawake ambao hapo kabla walikuwa wanaishi katika mahusiano yenye ukatili ndani yake. Hivyo kwa kutumia kifungu hiki mwanandoa ambaye anafanyiwa ukatili anaweza kuomba mahakama ili kutengana au kutalikiana na mwenzi wake.*

Kwa kutumia kifungu hiki, jamii hasa wanawake ambao ndiyo wahanga wa ukatili wa kijinsia wanaweza kuondokana na athari zinazoweza kutokea baada ya kufanyiwa ukatili. Athari hizo ni kama kujinyonga ama kuathirika kisaikolojia kwa sababu ya kuishi katika mazingira yenye ukatili maisha yao yote. Hii inawezekana kwa njia ya kuiomba Mahakama kuwatenganisha ama kutoa talaka kwa wanandoa hao.

*6.4.10 Haki ya Mgawanyo Sawa wa Mali ya Familia*

Kifungu cha 114(i) cha Sheria ya Ndoa ya 1971 kinatoa haki kwa wanandoa kupata mgawanyo sawa wa mali pale kunapokuwa na kutengana au talaka kwa amri ya mahakama. Hata hivyo wanawake wengi hawana uelewa juu ya haki kwani wamekuwa wakidhani kwamba hawana haki juu ya mali pale wanapoachana au kutengana.

*Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO), 2005 katika mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam, ulibaini kwamba asilimia 60 ya wanawake waliohojiwa walikiri kwamba wanapofanyiwa ukatili inabidi wasichukue hatua dhidi ya wenzi wao kwa kuhofia ndoa kuvunjika na wao kupoteza mali ya familia pamoja na watoto.*

Ifahamike kuwa, hata tafsiri ya kimahakama imekuwa kwamba, mwanamke ana haki ya kupata mgawo wa mali ya familia kwa usawa kabisa kama mwanaume hata kama hakuchangia moja kwa moja katika upatikanaji wake kwa maana ya kutoa pesa. Uwepo wake nyumbani kama mke wa kupika na kutunza watoto ni mchango tosha kabisa wa upatikanaji wa mali ya familia.

*6.4.11 Wajibu na Haki ya Matunzo ya Mwenza Baada ya Kuvunjika kwa Ndoa*

Kifungu cha 115 cha Sheria hii kinaelezea mamlaka ya Mahakama katika kuamuru, matunzo kwa mwenza. Sheria inatamka kuwa, Mahakama inaweza ikaamuru mume kutoa matunzo kwa mkewe au mtalaka wake (kati ya mambo mengine):-

a) Kama atakuwa amekataa au amepuuzia kutoa matunzo kama inavyoagizwa na sheria hii;
b) Kama amemtoroka, na kadri utoro huo utakavyokuwa unaendelea;
c) Wakati wowote ambapo taratibu za ndoa zitakavyokuwa zinaendela;
d) Wakati wa kutoa au baada ya kutoa amri ya kutengana;
e) Wakati wa kutoa au baada ya kutoa amri ya talaka; na
f) Pale ambapo wahusika walioana katika ndoa ya kiislamu, kwa wakati wa eda, kufuatia tarehe ya talaka au inavyochukuliwa kwamba imetolewa.

*Vilevile ifahamike kuwa, Mahakama itakuwa na mamlaka ya kukubaliana kumwamuru mwanamke kulipa gharama ya matunzo kwa mumewe au mtalaka wake pale ambapo hana uwezo kitimilifu au kwa kiasi fulani wa kujipatia kipato cha kuendesha maisha yake kutokana na kuumia kiakili, kimwili au afya mbaya (ugonjwa).*

*6.4.12 Haki na Wajibu wa Matunzo ya Mtoto Baada ya Ndoa Kuvunjika*

Kifungu 125 cha Sheria ya Ndoa ya 1971 kinatamka kuwa, Mahakama ina uwezo wa kuamuru uangalizi na matunzo ya mtoto pale ndoa inapovunjika.

Kwa mujibu wa sheria hii, Mahakama inaweza, wakati wowote kwa amri, kumweka mtoto chini ya ulinzi wa baba au mama yake au pale ambapo kuna mazingira maalumu inayofanya kutokuwa na imani na usalama wa mtoto huyo chini ya wazazi wa pande zote mbili, au ndugu yeyote wa mtoto huyo au shirikisho kwa minajili ya ustawi wa mtoto.

Katika kuamua ni nani awe mlinzi wa mtoto, uzingatiaji mkubwa utakuwa ustawi wa mtoto. Hivyo basi, Mahakama itazingatia: -

a) Matakwa ya wazazi wa mtoto;
b) Matakwa ya mtoto, pale ambapo amefikia umri wa kuweza kujieleza na kutoa maoni yanayo jitegemea; na
c) Mila ya jamii ya wahusika.

Pale ambapo kuna watoto wawili au zaidi katika ndoa, Mahakama haitalazimika kuwaweka wote chini ya uangalizi wa mtu mmoja bali itaangalia ustawi wa kila mtoto tofauti.

*Kwa kuwa ni dhana inayokubalika kwamba ni vizuri mtoto mwenye umri chini ya miaka saba awe chini ya uangalizi wa baba au mama yake, katika kuamua kama dhana hiyo inakubaliana na ukweli kuhusu kesi husika, mahakama itaangalia athari ya kumsumbua mtoto kwa kumbadilishia ulinzi.*

## 6.5 SHERIA ZA ARDHI ZA MWAKA 1999

Ardhi kama rasirimali kuu ya kiuchumi na kijamii inasimamiwa na kuratibiwa na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Mwaka 1999. Kutungwa kwa sheria hizi mbili kumetoa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika kupata, kumiliki, kutumia na kugawa ardhi. Baadhi ya haki zilizotajwa katika sheria hizi mbili ni: -

*6.5.1 Haki ya Kumiliki Ardhi*

Sheria hizi zinatamka wazi haki ya kupata na kumiliki ardhi sawa kwa mwanamke na kwa masharti yaleyale kama ilivyo kwa mwanaume na kuhakikisha kwamba miliki za ardhi zinalindwa na kutambuliwa kisheria.

*6.5.2 Haki sawa katika Maamuzi ya Ardhi*

Sheria imeweka wazi suala la maamuzi yanayohusiana na ardhi kwa kuzingatia jinsi. Wanawake wanashirikishwa katika Baraza la Ardhi la Taifa lenye wajumbe saba (7) angalau watatu (3) kati yao wawe ni wanawake. Halmashauri ya kijiji inatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua kumi na tano na wasiozidi ishirini na tano (15 – 25) kati yao theluthi moja (1/3 )wanatakiwa wawe wanawake.

*6.5.3 Wajibu wa Kupata Ridhaa ya Mwenza*

Sheria zimetoa mwongozo kwa Kamishina wa Ardhi na Halmashauri ya kijiji kutotoa idhini ya mtu kuhamisha au kuuza ardhi yake mpaka hapo itakapothibitishwa kuwa muuzaji amepata ridhaa toka kwa mwanandoa mwenzake. Hii ni haki inayoondoa unyanyasaji uliokuwa unafanywa na wanaume wengi ambao kwa kiasi kikubwa ndio wanaouza ardhi pasipo kuwajali wake zao na hivyo mwisho wa siku familia kukosa makazi.

*6.5.4 Wajibu wa Kutotumia Mila Potofu Kukandamiza Wanawake*

Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999 kinakataza matumizi ya kanuni ya mila kandamizi dhidi ya wanawake. Kifungu hicho kinabainisha kuwa, maamuzi yoyote yanayoingiwa kuhusiana na ardhi iliyo chini ya umiliki wa kimila yatakuwa ni batili na hayawezi kutekelezwa chombo chochote kile cha kisheria kwa njia au nia ya kuwanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu haki ya kupata au kumiliki au kutumia ardhi kwa namna yoyote ile ambayo kisheria ni halali.

## 6.6 SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO KAZINI, 2004

Sheria hii imeainisha haki na wajibu wa mfanyakazi pamoja na masuala mengine yahusuyo ajira. Hivyo imetoa miongozo ya kazi kwa wafanyakazi na waajiri kuhusiana na suala zima la ajira.

Ili kulinda haki ya wafanyakazi hasa wanawake ambao hapo awali wengi wao walikuwa wakibaguliwa katika masuala ya kazi na ajira, Sheria hii imetoa miongozo ifuatayo:

*6.6.1 Usawa Sehemu za Kazi*

Sheria hii inaelekeza kwamba mfanyakazi ana haki ya kutobaguliwa katika sehemu za kazi kwa namna yoyote ile. Hivyo ni wajibu wa mwajiri kuzingatia usawa katika ajira na wakati wowote ahakikishe kuwa hakuna ubaguzi katika sera ya ajira au katika masuala yoyote yanayohusiana na ajira kwa mfano katika kutangaza kazi au kuajiri wafanyakazi, mafunzo na maendeleo, uhamisho, adhabu na kadhalika.

*6.6.2 Mapumziko ya Uzazi*

Sheria inatoa haki ya mwanamke mfanyakazi aliyejifungua, kuwa ana haki zifuatazo:-

a) Ana haki ya kutofanya kazi ndani ya wiki sita tangu ajifungue isipokuwa kwa ruhusa ya daktari.
b) Ana haki ya kuendelea na kazi yake kwa mkataba uleule aliokuwa nao kabla ya kwenda likizo ya uzazi.
c) Ana haki ya kupewa likizo ya malipo angalau siku themanini na nne (84) au likizo ya siku mia moja (100) ikiwa atakuwa amejifungua watoto mapacha.
d) Ana haki ya kupewa siku themanini na nne (84) zaidi za likizo ya malipo ya uzazi ndani ya mzunguko wa likizo kama mtoto aliyemzaa atakufa ndani ya mwaka mmoja tangu azaliwe.

*6.6.3 Wajibu wa Kuzingatia Afya ya Mama Mjamzito na Mtoto*

Sheria hii mbali na kutoa haki kwa mwanamke mfanyakazi aliyejifungua pia inaeleza wajibu wa mwajiri katika kipindi cha mapumziko ya uzazi ikiwa ni pamoja na:-

a) Kumtaka au kutomruhusu mfanyakazi mjamzito au anayenyonyesha kufanya kazi ambazo zina uwezekano wa kuathiri afya yake au ya mtoto.
b) Kuweka makubaliano na mfanyakazi mwenye ujauzito au mwenye mtoto iwapo atamhitaji mfanyakazi huyo kufanya kazi katika mazingira yanayoweza kuhatarisha afya yake na ya mtoto.
c) Kumruhusu mfanyakazi anayenyonyesha kwenda kumnyonyesha mtoto kwa masaa mawili ambayo ni ndani ya masaa ya kazi.
d) Kutomtaka au kumruhusu mama mjamzito kufanya kazi masaa ya usiku.

Hata hivyo amri hii haimbani mwajiri ikiwa mfanyakazi ataomba kufanya kazi na ikiwa ataonyesha cheti cha matibabu kinachothibitisha uimara wa afya yake au ya mtoto na kwamba kufanya kazi hakuta muathiri afya yake au ya mtoto.

*Amri hii ya kisheria kwa mjamzito kutokufanya kazi usiku ni katika kipindi cha miezi miwili kabla ya kujifungua na miezi miwili baada ya kujifungua ikiwa mama huyo ataonyesha cheti cha matibabu chenye kuthibitisha kuwa afya yake au ya mtoto haimruhusu kufanya kazi za usiku.*

## 6.7 SHERIA YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA VVU NA UKIMWI YA 2008

Sheria hii imetungwa ili kujaribu kuzuia na kupambana na ueneaji wa maambukizi wa VVU/UKIMWI pia kama sehemu ya utekelezaji wa malengo ya sera ya UKIMWI tuliyoizungumzia hapo juu. Sheria hii imetungwa mwaka 2008, na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache sana duniani zenye sheria maalumu kwa ajili ya kuzungumzia masuala ya gonjwa hili.

*6.7.1 Majukumu ya Kisheria Kuhusu UKIMWI*

Kifungu cha 4 na vingine vinatamka kuwa, kila mtu, taasisi na asasi anayeishi au zilizosajiliwa na zinafanya kazi Tanzania, zinatakiwa kutekeleza haya yafuatayo -

a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu vyanzo vya maambukizi ya UKIMWI, aina ya uambukizaji, matokeo yake, kuzuia, nk.
b) Kupunguza kuenea kwa UKIMWI na VVU, Magonjwa yanayoambukizwa kwa kujamiiana, nk.
c) Kulinda haki za yatima kwa kutoa huduma za afya na za kijamii, kukataza upimaji wa lazima, kupambana na unyanyapaa na kubaguliwa.
d) Kuibua/pinga mila potofu zinazochochea ueneaji wa UKIMWI katika jamii.
e) Kuhimiza mila zote ambazo zinaweza kuchangia/kutumika katika kupunguza maambukizo ya UKIMWI.

f) Kuongeza upatikanaji, huduma na msaada kwa watu wanaoishi na UKIMWI kutoka katika jamii ama nyenzo za huduma ya afya
g) Kulifanya suala la UKIMWI kama mtambuka katika programu zote za watu wote. Kila mwajili aandae programu maalumu katika sehemu za kazi kuhusu UKIMWI.
h) Mashirika yote ya UKIMWI yenye majukumu hayo, yanawajibika kuitaarifu TACAIDS kuhusu mipango yao kwa ajili ya kuepuka mgongano wa rasilimali katika eneo moja tu.
i) Kuhusu elimu kwa umma (kifungu cha 8), sheria inaelekeza kuwa itolewe katika mfumo ulio sahihi na unaoweza kufikisha ujumbe kwa watu wote (hata walemavu, watoto na wanawake).
j) Serikali kuwasomesha wahudumu katika sekta ya afya.
k) Kuchangia na kutunza damu salama katika benki za damu.
l) Kupimwa watu UKIMWI – vituo vyote vya huduma za afya vya serikali vimetajwa kuwa ni kwa ajili ya kupima pia.
m) Vituo vya huduma ya afya ni lazima viwe rafiki wa watu wenye ulemavu na viwe na wataalamu waliofunzwa katika masuala ya ushauri/ nasaha.
n) Kutunza siri za wagonjwa.

*6.7.2 Haki ya Kupima*

Kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya UKIMWI, kinakataza upimaji wa nguvu. Hivyo mtu ni lazima aridhie yeye mwenyewe kwenda kupimwa. Kuhusu watu wasiojiweza kiakili ama watoto, Kifungu cha 15(2) kinasema kuwa, mtoto au mtu yoyote asiyeweza kutambua majibu yake baada ya kupima, atapimwa pale tu pale ambapo kutakuwa na ruksa ya maandishi ya mzazi wake ama mtu anayetambulika kisheria kuwa ni mlezi wake.

*Kiujumla suala la kupima ni la hiari. Sheria inasema kuwa itakuwa ni marufuku kwa Afisa afya [ama mtu/ taasisi nyingine] kumlazimisha mtu kupima. HATA HIVYO, kwa akina mama wenye ujauzito na akina baba wanaohusika na ujauzito huo, ni lazima watapewa huduma ya ushauri na wakiona wako tayari, wanatakiwa kupima. Pia kwa mtu ambaye hajiwezi kabisa, anaweza kupimwa bila kupata ruksa zilizotajwa.*

*6.7.3 Haki ya Kupata Majibu ya Upimaji*

Kuhusu kupata majibu ya upimaji, Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya UKIMWI kinasema kuwa, majibu ni lazima yatolewe kwa usiri kwa mtu aliyepima, tena pale mtu atakapo hiari kupokea majibu yake.

*Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 16(2) cha sheria hiyo, majibu yanaweza kutolewa kwa mtu asiyehusika (ambaye siye aliyepima) endapo; mtu aliyepimwa ni mtoto, ambapo mzazi ama mlezi anaweza kuchukua majibu yake; mtu ambaye hawezi kupokea kutokana pengine na woga ila ana nia hiyo, mwenza wake ama mlezi wake anaweza kumpokelea; na mtu aliyepimwa ni mwanandoa ama rafiki wa kimapenzi, mwenza wake anaweza kupokea majibu ya mwenzake.*

*6.7.4 Haki ya Usiri wa Majibu*

Kifungu cha 17 (1) cha Sheria ya UKIMWI kinawakataza wahudumu wa afya, wafanyakazi, watumishi, wakala wa ajila, wakala wa bima, watunza kumbukumbu, watafsiri lugha za alama, walezi, na watu wengine kuzingatia amri hii ya kutunza siri za hali ya mtu hasa aliyeambukizwa VVU/UKIMWI, hata kama amekufa.

*Hata hivyo, amri hiyo inaweza kutokuzingatiwa (kisheria) kwa sababu ya; kutimiza wajibu wa utoaji taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathimini; kuwajulisha wauguzi wengine watakao muhudumia mgojwa huyo (ili waepuke maambukizi); kutimiza amri ya Mahakama kutokana na shauri lililoko Mahakamani linalohusu hali ya muhusika; na kutoa taarifa kwa mtu husika wa familia ya marehemu.*

*6.7.5 Haki Dhidi ya Unyanyapaa na Ubaguzi kutokana na UKIMWI*

Kifungu cha 28 cha Sheria ya UKIMWI kinakataza utungwaji wa sera (ngazi yeyote), ama sheria ama kitendo chochote ambacho kwa tasfiri yake kitaleta unyanyapaa ama ubaguzi dhidi ya mtu mwenye UKIMWI. Kifungu cha 29 kinawataka wauguzi wanaoshughulikia wagonjwa wa UKIMWI kutoa huduma bila unyanyapaa ama ubaguzi wa aina yeyote ile.

Sheria imetoa adhabu ya faini ya hadi shilingi 2,000,000 au kifungo cha mwaka mmoja jela kwa mtu atakayetenda kosa/ makosa haya.

*Kifungu cha 30 kinakataza mambo mengine/ aina nyingine za ubaguzi. Kinasema kuwa, ni marufuku; kumnyima mtu usajili, ushiriki katika huduma yeyote ama kumfukuza mtu kutoka katika taasisi; kumzuia mtu kusafiri ndani ama nje ya Tanzania; kumnyima mtu fursa ya ajira; kumkataza mtu kuishi popote, au kumkataza mtu ukaazi kwa sababu ya hali yake ya ugonjwa wa UKIMWI.*

*6.7.6 Kuambukiza UKIMWI kwa Makusudi*

Kifungu cha 47 cha Sheria ya UKIMWI kinakataza uambukizaji wa maksudi wa ugojnwa wa UKIMWI/VVU kwa mtu mwingine (intentional transmission of HIV to another person). Mtu akipatikana na hatia ya kutenda kosa hili, adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka mitano jela ama kisichozidi miaka kumi jela.

*6.7.7 Ulinzi wa Haki za Watoto dhidi ya VVU/UKIMWI*

Kifungu cha 19 kinasema kuwa serikali, kwa kutumia rasilimali tulizopo, italazimika kuhakikisha kuwa kila mtu anayeishi na UKIMWI/VVU, watoto walio katika hatari ya kuathirika, watoto yatima wanapata huduma za msingi.

Kifungu cha 25 kinakataza maambukizo ya UKIMWI toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Kifungu hiki kinasema kuwa, katika kupambana na hili, Wizara ya Afya itasimamia huduma na matibabu yanayomuhusu mwanamke mwenye mimba.

Kifungu cha 27 kinaainisha kuwa, majibu yoyote ya vipimo ya VVU/UKIMWI ni lazima yahakikiwe kwanza kabla ya kutangazwa/ kutolewa. Hii inasadia sana kutotoa majibu yasiyo sahahi ambayo yanaweza kuleta wasiwasi kwa wazazi na watoto.

SURA YA

7




# Kitendo cha Ukatili wa Kijinsia kama Kosa la Jinai

# KITENDO CHA UKATILI WA KIJINSIA KAMA KOSA LA JINAI

## 7.1 UTANGULIZI

Matukio mengi au vitendo vingi vilivyotajwa katika sura zilizopita ambayo ni ukatili wa kijinsia ni makosa ya jinai au husababisha makosa ya jinai ambao karibu yote huadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania. Hata hivyo, kuna baadhi ya vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia matokeo yake ni kosa la daawa (madai) na mengine, ni mchanganyiko wa jinai na daawa. Kwa mfano, kitendo cha kumdhihaki mwanamke, ni jinai lakini pia ni daawa.

## 7.2 SHERIA YA KANUNI ZA ADHABU, SURA YA 16

Sheria hii ndiyo kuu inayoshughulikia na kusimamia makosa ya jinai katika nchi yetu. Makosa yenye asili ya jinai kama yalivyoainishwa katika sheria hii yanalenga kutoa adhabu kwa jinsi zote, yaani wanawake na wanaume endapo watapatikana na hatia ya uvunjifu wa kifungu husika.

*Ili kulinda utu na heshima za wanawake na watoto, Sheria hii ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ilifanyiwa marekebisho mwaka 1998 na kutoa adhabu kali katika makosa ya kujamiiana. Marekebisho haya yaliingizwa na kuwa sehemu ya Sheria ya Kanuni za Adhabu mwaka 2002. Vipengele vilivyoboreshwa pamoja na vipengele vingine vinatoa adhabu kali katika makosa ya jinai ingawa havijawalenga wanawake moja kwa moja.*

Japokuwa ukatili wa kijinsia haujatamkwa moja kwa moja kuwa ni kosa la jinai, namna ambayo hutokea na matokeo yake huakisiana na aina ya makosa ya jinai ambayo yametajwa na sheria hii kama ambavyo imejadiliwa hapa chini katika sura hii.

### *7.2.1 Lugha ya Matusi, Mzozo na Vitisho*

Kifungu cha 89 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kinakataza mtu yeyote kutumia lugha chafu au kutukana mtu yeyote kwa lengo la kuvunja amani. Kitendo hiki ni kosa la jinai na mtu yeyote atakayefanya hivi atahukumiwa jela kifungo cha miezi sita. Lugha za vitisho na matusi zimekuwa zikitumika kwa kiasi kikubwa katika jamii na hasa kwa lengo la kudhihaki na kutweza utu wa mwanamke na mtoto.

*Wanawake wengi wamekuwa wakikatazwa au kunyimwa ruhusa ya kufanya kazi, biashara au kujishughulisha na shughuli ndogondogo za kimaendeleo. Huu ni ukatili wa kijinsia na ni kosa la jinai kufanya hivyo.*

Kifungu hiki pia kimekataza mtu yeyote kuchungulia au kuzonga sehemu yoyote kwa lengo la kumzuia mtu mwingine kufanya kitendo ambacho kisheria angeweza kufanya au kumshurutisha mtu yeyote kufanya kitendo ambacho kisheria asingeruhusiwa kufanya.

### *7.2.2 Kosa la Kubaka*

Kifungu cha 130 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kinakataza kitendo hiki. Dhana nzima ya kosa la kubaka na mazingira mbalimbali ambapo ubakaji unaweza kufanyika yameainishwa katika kifungu hiki.

Tafsiri ya neno mwanamke katika kifungu hiki inamaanisha kuwa mwanamke ni mtu yeyote mwenye jinsi ya kike bila kujali umri. Kwa mantiki hiyo, hata mtoto wa mwaka mmoja mwenye jinsi ya kike kwa tafsiri ya kifungu hiki ni mwanamke. Hivyo basi, ni kosa la jinai kwa mwanaume kumwingilia au kujamiiana na mwanamke, katika mazingira yafuatayo:-

a) Kumwingilia au kujamiiana na mwanamke ambaye si mke wake bila ridhaa yake au hata kama ni mke wake waliyetengana naye.
b) Kujamiiana na mwanamke kwa ridhaa yake ambapo ridhaa hiyo imepatikana kwa matumizi ya nguvu, vitisho au kwa kumweka mwanamke huyo kwenye hatari (hofu) ya kifo au kumuumiza au kama mwanamke huyo atakuwa amewekwa kwenye kizuizi kinyume cha sheria.
c) Kujamiiana na mwanamke kwa ridhaa yake iwapo ridhaa hiyo imepatikana wakati mwanamke huyo hakuwa na akili timamu au alikuwa katika hali ya ulevi aliopewa kwa aina yoyote ya madawa au kitu chochote alichopewa na mwanaume au na watu wengine.
d) Endapo ridhaa hiyo imetolewa na mwanamke kwa mwanamume aliyeigiza na kujifanya mume halali wa mwanamke au msichana huyo na kupelekea kuamini ni mume wake halali.
e) Kujamiiana kwa ridhaa au bila ridhaa na mwanamke wa chini ya miaka 18 vinginevyo basi huyo

mwanamke awe ni mke wake ambaye ni wa miaka 15 au zaidi na hawakutengana.

Sheria hii imedhibiti makundi mbalimbali katika jamii ambayo kwa nafasi zao huweza kutumia mwanya huo na hivyo kupelekea kutenda makosa ya kujamiiana, kama ifuatavo, kwamba, mtu yeyote:-

a) Ambaye yuko katika nafasi ya mamlaka na akatumia nafasi hiyo ya kiofisi na kumbaka mwanamke katika mahusiano ya kiofisi au kumzuia kinyume cha sheria ili ajamiiane naye atakuwa ametenda kosa la jinai.
b) Ambaye yuko katika nafasi ya kiutawala au mtumishi katika sehemu za kuhifadhiwa watoto wahalifu au sehemu zozote za hifadhi zilizoanzishwa kisheria na akatumia nafasi hiyo kubaka atakuwa ametenda kosa la jinai.
c) Ambaye yuko katika nafasi ya utawala au mtumishi wa hospitali na akatumia nafasi yake kumbaka mwanamke atakuwa ametenda kosa la jinai.
d) Ambaye ni mganga wa kienyeji na akatumia nafasi yake kumbaka mteja wake anayempa matibabu, basi atakuwa ametenda kosa la jinai.
e) Ambaye ni kiongozi wa dini akatumia nafasi yake kumbaka mwanamke atakuwa ametenda kosa la jinai.

*7.2.3 Bughudha/ Shambulio la Kijinsia*

Kifungu cha 135 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kinaeleza bayana kwamba mtu yeyote ambaye kwa dhamira akamshambulia, au akatumia nguvu kinyume cha sheria kumbughudhi mtu mwingine kijinsia au kwa kutumia maneno au vitendo na kusababisha maudhi au bughudha za kijinsia kwa mtu mwingine, basi mtu huyo atakuwa ametenda kosa la bughudha za kijinsia.

*7.2.4 Unyanyasaji Wa Kijinsia Dhidi ya Watoto*

Sheria hii hasa katika Kifungu cha 138B imeainisha mazingira mbalimbali ambayo kosa la unyonyaji wa kijinsia dhidi ya mtoto linaweza kutendeka kwa mfano kwa kumchukua au kumruhusu mtoto yeyote kukaa katika maeneo yake kwa lengo la mtoto huyo kutumiwa vibaya kwa matendo ya kujamiiana, kufanya maonyesho kinyume cha maadili, atakuwa ametenda kosa la unyonyaji dhidi ya watoto.

*7.2.5 Shambulio la Aibu kwa Wanawake*

Mtu yeyote kwa kudhamiria akasababisha maudhi ya kijinsia kwa mwanamke ama kwa kumtamkia maneno au kutoa sauti, ishara au kuonyesha maneno au kitu chochote kwa nia kwamba maneno hayo au sauti hiyo iweze kusikika au ishara au kitu hicho kiweze kuonekana na mlengwa, basi mtu huyo atakayefanya moja kati ya maudhi hayo atakuwa ametenda kosa la shambulio la kijinsia na shambulio la aibu kwa wanawake.

*Endapo shauri hili la shambulio la aibu litafikishwa mahakamani, na mwathirika akawa ni mtoto wa kiume au wa kike chini ya miaka 18, sheria inatamka bayana kuwa haitakuwa kinga hata kama mtoto huyo atakuwa aliridhia kufanyiwa vitendo hivyo.*

*7.2.6 Matendo Yanayokiuka Maadili kwa Kiwango cha Juu*

Kifungu cha 138 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kinasemakuwa mtu yeyote ambaye katika hadhara au faragha akatenda matendo yanayokiuka maadili kwa kiwango cha juu au akawa sehemu katika utendaji wa matendo yanayokiuka maadili, kisheria atakuwa ametenda kosa la jinai.

*7.2.7 Ukiukwaji wa kijinsia Wa Kiwango Cha Juu*

Mtu yeyote ambaye ili kuridhisha tamaa ya kimwili akafanya kitendo chochote kwa kutumia kiungo chake cha kijinsi au kiungo chochote cha mwili wake au kifaa chochote cha mtu mwingine ambacho kitendo hicho hakitambuliki kwa tafsiri ya sheria hii kuitwa kitendo cha kubaka, basi atakuwa ametenda kosa la ukiukwaji wa kijinsia wa kiwango cha juu. Vitendo vinavyoharamishwa chini ya kosa hili ni:-

a) Vitendo vinavyofanywa bila idhini ya mtendewa.
b) Kwa ridhaa ya mtendewa lakini ridhaa hiyo imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho au kumweka mtu huyo katika hofu ya kifo au kuumia au wakati mwathirika yuko katika kizuizi kinyume cha sheria.
c) Kwa ridhaa ya mtendewa ambapo ridhaa hiyo imepatikana wakati mtendewa hakuwa na akili timamu au alikuwa katika hali ya ulevi uliosababishwa na pombe au madawa ya kulevya au kitu kingine chochote.

*7.2.8 Kujamiiana Kinyume na Maumbile*

Mtu yeyote ambaye atajamiiana na mtu mwingine kinyume na maumbile au akajamiiana na mwanaume au kamruhusu mwanamume kumwingilia kinyume na maumbile, au kufanya tendo la kujamiiana na mnyama, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la jinai..

*7.2.9 Makosa ya Maharimu kwa Wanaume*

Mwanaume yeyote ambaye atakuwa na mahusiano ya kujamiiana na mwanamke huku akifahamu kuwa ni mjukuu wake, binti yake, dada au mama yake basi kisheria atakuwa ametenda kosa la maharimu kwa wanaume.

*7.2.10 Makosa ya Maharimu kwa Wanawake*

Mwanamke yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi ambaye kwa ridhaa yake atamruhusu babu yake, baba yake, kaka au mtoto wake wa kiume kujamiiana naye, basi kisheria atakuwa ametenda kosa la maharimu kwa wanawake.

*7.2.11 Kosa la Kutelekeza Mtoto kwa Makusudi*

Vifungu vya 166 na 167 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 Kwa mujibu wa vifungu hivi mtu ambaye ni mzazi au mlezi au mtu yeyote ambaye ana dhamana ya kumtunza mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne (14) na kwa makusudi na pasipo sababu yoyote ya msingi akamtelekeza bila kuwepo msaada wowote atakuwa ametenda kosa la jinai.

*Kifungu hiki kikitumika vizuri kinaweza kuepusha ongezeko la watoto wa mitaani na hasa watoto wa kike ambao wanaweza kuingia katika matendo mabaya ikiwa ni pamoja na kujiingiza katika masuala ya ngono ili kupata unafuu wa maisha ambapo athari zake ni kuharibikiwa utu wao, kupata mimba zisizotarajiwa na hata kuambukizwa magonjwa ya zinaa na VVU/UKIMWI.*

*7.2.12 Kosa la Kutesa na Kukeketa*

Kifungu cha 169A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kinatoa kosa kwa mtu yeyote ambaye ana dhamana ya kumtunza au mwangalizi wa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, kumtesa, kumtelekeza au kumkeketa ama kupelekea mtu huyo kuteseka, kuteswa au kutelekezwa kwa lengo la kudhuru afya yake.

*Madhara ya afya yanaweza kuwa kwa njia ya kushindwa kuona, kusikia ama kupoteza viungo vya mwili au kupata ugonjwa wa akili na hivyo atakuwa ametenda kosa la jinai. Kifungu hiki kikitumiwa vizuri kinaweza kupunguza au kutokomeza athari zinazotokana na kuteswa, kutelekezwa na kukeketwa kwa watoto wa kike ambao huwaletea madhara ya kiafya hivyo kupelekea kujifungua kwa shida.*

SURA YA

# 8




# Vyombo vya Usimamizi wa Haki Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

# VYOMBO VYA USIMAMIZI WA HAKI DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA

## 8.1 UTANGULIZI

Ili kuhakikisha haki za binadamu zinatekelezwa kwa mujibu wa masharti na viwango husika,, ikiwa ni pamoja na kumlinda mwanamke dhidi ya ukatili wa kijinsia, vimewekwa vyombo mbali mbali kwa lengo la usimamizi wa masharti ya sheria. Katika ngazi ya kimataifa/kikanda, vyombo hivyo vimeundwa na mikataba ya kimataifa/kikanda ya haki za binadamu. Katika ngazi ya nchi vyombo vya utekeleaji vinaundwa na katiba ya nchi pamoja na sheria mbalimbali.

## 8.2 USIMAMIZI NGAZI YA KIMATAIFA

Vyombo vya kusimamia utekelezaji wa Haki za Binadamu kimataifa vinaundwa kulingana na mkataba husika. Mfano chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa 1979, kuna Kamati ya Kimataifa ya Usimamizi wa CEDAW.

Kazi ya Kamati hiyo pamoja na; (i) kupokea na kuchambua ripoti za utekelezaji wa haki za binadamu kutoka katika kila nchi mwanachama wa Mkataba huu ambapo Tanzania hutakiwa kuwasilisha kila baada ya miaka minne. (ii) Kutolea maamuzi hasa kuhusu mapungufu na kuagiza nchi husika kufanya jitihada zaidi. Vyombo vingine vya kimataifa ni kama Kamati ya Kuondoa Ubaguzi wa Rangi, Kamati ya Watoto, Kamati ya Kuziua Utesaji, na kadhalika.

## 8.3 USIMAMIZI NGAZI YA KIKANDA - AFRIKA

Kanda zinazozungumziwa katika ulingo wa haki za binadamu ni kama Ulaya, Amerika, na Afrika. Katika ngazi ya Afrika, chombo cha kusimamia utekelezaji hadi sasa ni Tume ya Haki za Binadamu na Watu iliyoundwa chini ya Ibara ya 30 ya Mkataba wa Kiafrika wa Haki za Binadamu na Watu wa 1981. Inaundwa na Wajumbe 11 kutoka nchi wanachama wa mkataba huu.

Nchi wanachama wa mkataba huu zinawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Haki za Binadmau kila baada ya miaka miwili (2). Pia nchi wanachama wa Mkataba huu zina haki ya kupeleka malalamiko yake katika tume hii dhidi ya nchi nyingine wanachama. Vile vile Asasi za Kiraia (AZAKI) na watu binafsi wanaweza kupeleka malalamiko yao mbele ya Tume ili mradi malalamiko hayo yamekwisha sikilizwa na vyombo vya kutoa maamuzi vilivyoko ndani ya nchi husika na utatuzi wake haukupatikana au imekuwa si rahisi kupata ufumbuzi wa ndani.

Mfano Mtanzania aliyekiukiwa haki yake chini ya mkataba anaweza tu kupeleka lalamiko lake mbele ya Tume hii ikiwa tu suala lake limekwisha amuliwa na Mahakama ya Rufaa, au kama haikuwezekana kupata maamuzi ya mahakama kutokana na ucheleweshwaji wa kupindukia na kadhalika.

## 8.4 USIMAMIZI KITAIFA - TANZANIA

Nchini mwetu haki za binadamu zimewekwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, sehemu ya III ya sura ya kwanza Ibara ya 12 - 29. Vilevile, kama ilivyoainishwa katika sura zilizopita za kitabu hiki, sheria mbalimbali zimetamka kuwa vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia ni makosa ya jinai na daawa (madai).

Hivyo, mhanga wa ukatili wa kijinsia au ukiukwaji wa haki zake kama binadamu anaweza kumshitaki mlalamikiwa na/au kudai fidia kwa njia zifuatazo:

### *8.4.1 Kufungua Shauri la Kikatiba/ Haki za Binadamu*

Chini ya Ibara ya 30 (b) mtu yeyote anayedai kukiukiwa haki yake anaweza kufungua shauri la kudai haki hiyo Mahakama Kuu ya Tanzania.

Kesi ya aina hii husikilizwa na Majaji watatu wa Mahakama Kuu baada ya kuidhinishwa na Jaji mmoja wa Mahakama hiyo, kwamba kweli ni kesi inayoweza kusikilizwa. Ikiwa Mahakama baada ya kusikiliza shauri ikiridhika kwamba haki imekiukwa itatoa amri kwamba haki hiyo itekelezwe au fidia ilipwe kulingana na madhara yaliyofanyika.

*8.4.2 Kufungua Shauri la Kutendewa Kosa la Jinai*

Hii inaweza kufanyika kwa kutoa taarifa katika kituo chochote cha polisi karibu na tukio lilipotokea. Katika kesi za namna hii, mlalamikaji anakuwa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mhanga wa tukio la ukatili wa kijinsia anakuwa ni kama shahidi muhimu wa kesi hiyo.

*Ifahamike kuwa, kwa mujibu wa Ibara ya 26(2) ya Katiba ya Tanzania na Kifungu cha 7 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya 1985, kila mtu ana wajibu wa kusimamia sheria za nchi. Hivyo basi, kila mtu kwa nafasi yake anatakiwa kutaarifu Jeshi la Polisi la Tanzania au mamlaka nyingine yeyote ya kisheria juu ya ukatili wa kijinsia na vilevile, kusaidia katika upatikanaji wa haki kwa kutoa ushahidi au ushauri pale itakapobidi.*

*8.4.3 Kufungua Shauri la Daawa/ Madai*

Hii inaweza kufanyika kwa kwa kufungua/ wasilisha hati ya madai katika Mahakama yeyote ya Tanzania kutegemeana na kiwango cha madai (thamani ya fidia), eneo lilipotokea tukio na aina ya mlalamikiwa. Kesi ya madai inaweza kufunguliwa na muhanga wa tukio la ukatili wa kijinsia au mwakilishi wake kisheria kamavile wakili, mlezi ama jamaa husika.

*Ifahamike kuwa, mlalamikiwa anaweza kushitakiwa kwa kosa la jinai na kwa kosa la daawa kwa wakati mmoja. Sheria inaruhusu hali hii. Hivyo, mhanga wa kosa la ukatili wa kijinsia anaweza kushitaki katika Jeshi la Polisi kwa kosa la jinai lakini pia, kwa kosa hilo hilo, anaweza kupeleka madai ya daawa ili kupata fidia.*

*8.4.4 Kufungua/ Peleka Lalamiko Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora*

Mbali na njia hizo, mhanga anaweza kutoa au peleka malalamiko ya kuvunjiwa haki zake kama binadamu kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo kwa mujibu wa sheria yake ya mwaka 2001, ina wajibu na nguvu kisheria ya kushughulikia aina zote za ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na masuala ya ukatili wa kijinsia.

Tume hii, inaweza kufanya uchunguzi, kumuita mdaiwa na hata kutoa mapendekezo ya utekelezaji wa maamuzi yake. Endapo mdaiwa atakaidi uamuzi wa Tume, anaweza kushitakiwa Mahakamani na Tume yenyewe au mlalamikaji.

SURA YA

9




# Jitihada, Mafanikio na Changamoto za Juhudi Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

# JITIHADA, MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA JUHUDI DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA

## 9.1 UTANGULIZI

Kuna jitihada kadhaa, mafanikio na changamoto nyingi vitokanavyo na masuala ya ukatili wa kijinsia. Jitihada hizo zimekuwa zikifanywa na serikali pamoja na asasi za kiraia (AZAKi) kwa pamoja au kila mmoja kwa wakati wake. Ni harakati za muda mrefu sasa kumekuwa na jitihada hizo. Hata hivyo, zimejidhihirisha zaidi kuanzia kipindi cha miaka ya 1990 wakati mashirika kama WiLDAF Tanzania yalipoanza kumea kwa wingi hapa Tanzania.

## 9.2 JITIHADA ZILIZOFANYWA NA SERIKALI

### *9.2.1 Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000*

Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni mojawapo ya miongozo ya serikali katika jitihada za kuwapa wananchi mwelekeo wa maendeleo ya wanawake na jinsia utakaohakikisha kuwa sera, mipango, mikakati na shughuli mbalimbali za maendeleo katika kila sekta na taasisi katika ngazi zote zinazingatia usawa wa kijinsia.

Mwelekeo wa maendeleo kijamii, kitaifa na kimataifa hivi sasa unasisitiza na kuhimiza upangaji na utekelezaji mipango unaozingatia ushirikishwaji wa wanawake na wanaume kwa pamoja katika kutambua, kuthamini na kukuza vizuri zaidi uwezo wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao.

Ili kurahisisha na kuwezesha utekelezaji, sera imeelekeza kuwepo na vitengo vya jinsia katika muundo wa serikali kuu na serikali za mitaa na taasisi mbalimbali. Vile vile sera inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa chombo kisichofungamana na itikadi yoyote cha kuwaunganisha wanawake na kuishauri serikali.

### *9.2.2 Dira ya Maendelo ya Taifa ya Mwaka 2025*

Dira hii imelenga kuondoa umaskini wa kupindukia na kufanya Tanzania nchi yenye pato la wastani. Aidha kwa dira hii tunategemea kuona maisha bora na ya hali ya juu kwa wote, amani, utulivu na umoja, utawala bora, jamii iliyoelimika na uchumi imara wenye ushindani, endelevu na ya kuweza kufaidisha watu sawa wake kwa waume. Changamoto ni je, tutafikia lengo hilo kwa wakati muafaka?

### *9.2.3 Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana Umaskini Tanzania (MKUKUTA)*

MKUKUTA ni mkakati unaoweka kipaumbele katika kupunguza umaskini katika agenda ya maendeleo ya nchi. MKUKUTA umetokana na changamoto za Dira ya Maendeleo ya Taifa (Dira 2025) kwa maendeleo ya hali ya juu na shirikishi, maisha bora, amani, utulivu na umoja, utawala bora, elimu bora na ushindani wa kimataifa.

MKUKUTA inalenga kufikisha wadau kwenye malengo ya maendeleo ya milenia kama inayolenga kwenye makubaliano ya kimataifa ya kupunguza umaskini, njaa, maradhi, ujinga, uharibifu wa mazingira na ubaguzi dhidi ya wanawake ifikapo mwaka 2025. Inalengo katika ushiriki/ushirikishwaji wa AZAKi, maendeleo ya sekta binafsi na ushirikiano wenye manufaa wa ndani na nje kwenye nyanja ya maendeleo pamoja na jitihada za makusudi za kikanda na kimataifa kwa ajili ya kijamii na ya kiuchumi.

### *9.2.4 Jitihada Nyingine za Serikali*

Jitihada zingine zilizofanywa na serikali ni pamoja na:-

a) Serikali imetunga sheria zinazomtambua mwanamke na kuthamini uatu wake.
b) Serikali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali zinazomlenga mwanamke.
c) Nafasi za wanawake katika mamlaka mbalimbali zimeongezeka kufikia asilimia 30.
d) Kuwepo kwa wizara inayosimamia masuala ya jinsia.
e) Kuanzishwa kwa madawati ya jinsia kwenye idara mbalimbali za wizara katika ngazi za mikoa na wilaya.
f) Serikali imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayolinda hadhi ya wanawake kwa mfano CEDAW, Mkataba wa Maputo na kadhalika.
g) Viti maalum kwa wabunge wanawake.
h) Uanzishwaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

## 9.3 JITIHADA ZA ASASI ZA KIRAIA

a) Asasi za Kiraia (AZAKi) zimefanya kampeni za kuelimisha umma katika masuala ya jinsia kupitia njia mbalimbali kama vile machapisho; mafunzo kwa viongozi na jamii kwa ujumla; usimamizi wa utekelezaji wa haki za binadamu; na vyombo vya habari.

b) Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria na uwakilishi mahakamani.

c) AZAKi zimesaidia kufanya marekebisho ya sheria ambazo zinamgandamiza mwanamke.

d) Kushawishi kutungwa kwa sheria mpya zinazomtambua na kumlinda mwanamke. Kwa mfano, Sheria ya UKIMWI; Sheria ya Watoto; na kadhalika.

e) Kuibua mijadala mbalimbali ya kitaifa inayolenga utetezi wa usawa wa kijinsia.

f) Kutoa elimu juu ya haki za wanawake.

g) Wanaharakati wamekuwa wakifanya jitihada kadhaa ili kufuta sheria ya kimilaya mirathi ya mwaka1963 ambayo ni kandamizi kwa wanawake. Baadhi ya juhudi zilizofanyika ni kuunda kikosi kazi kinachojulikana kama KIKUHAMI, kikishirikisha mashirika mbalimbali chini ya uratibu wa WiLDAF. Jitihada nyingine zilizofanywa na kikosi kazi ni kuandaa rasimu mbadala ya sheria za mirathi, kufanya ushawishi katika wizara ya maendeleo yajamii, jinisa na watoto, wizara ya katiba na sheria, vyama vya siasa na kamati za Maendeleo ya Jamii pamoja na ile ya Katiba.

## 9.4 JITIHADA ZILIZOFANYWA NA JAMII

Jamii kama sehemu yenye wadau mbalimbali kama viongozi wa serikali za mitaa/vijiji, taasisi za dini, watoto wa shule, vikundi vya kijamii, watu wazima na kadhalika, imekuwa ikiyapokea na kuyafanyia kazi yale ambayo yamefanywa na serikali na mashirika katika kutetea haki za mwanamke. Kutokana na harakati mbalimbali kuhusu ukatili wa kijinsia, kumekuwa na mwamko wa kijamii wa kupambana na ukatili wa kijinsia.

## 9.5 JITIHADA ZA MASHIRIKA YA MAENDELEO/WAHISANI

Mashirika wahisani wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kwa serikali, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kutokomeza ukatili wa kijinsia. Misaada hii ni pamoja na fedha zinazotumika katika miradi mbalimbali yenye lengo la kupambana na ukatili wa kijinsia; kwa mfano fedha kwa ajili ya kazi za utetezi na zile za kujenga uelewa kuhusu suala zima la ukatili wa kijinsia.

Baadhi ya mashirika wahisani walio katika mstari wa mbele katika kusaidia juhudi za kupambana na ukatili wa kijinsia ni pamoja na Shirika la Msaada la Marekani (USAID), Shirika la Msaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Kanada (CIDA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Shirika la Misaada la Kanisa la Norway (NCA), Mfuko wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Maendeleo ya Wanawake (UNIFEM), Mfuko wa Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na kadhalika.

Mbali ya mashirika wahisani kutoa misaada ya fedha, pia wamekuwa wakishiriki moja kwa moja katika kampeni mbalimbali za kupambana na ukatili wa kijinsia kama zile za Kataa Ukatili wa Kijinsia, Tunaweza, Tamali, Siku 16 za Kupinga Ukatili wa kijinsia, nakadhalika.

## 9.6 BAADHI YA CHANGAMOTO

Pamoja na kuwepo kwa jitihada mbalimbali za kulinda Haki za Wanawake dhidi ya Ukatili wa Kijinsia nchini Tanzania ikiwamo kuweka sera na sheria mbalimbali zanazolinda hadhi ya wanawake, bado kuna changamoto katika mchakato wa utekelezaji pamoja na mambo mengine. Baadhi ya changamoto ambazo zinarudisha nyuma jitihada hizi ni kama ifuatavyo:

### *9.6.1 Mgongano wa Sheria*

Kumekuwa na mgongano wa sheria juu ya umri wa msichana anayepaswa kuolewa bila ya kuwepo shaka yoyote. Mgongano huu unahusisha ya Sheria Ndoa ya Mwaka 1971 inayotambua kwamba umri wa msichana kuolewa ni kuanzia miaka 16 ikiwa ni kwa ridhaa yake na anapotaka kuolewa akiwa na miaka 15 ni lazima apate ridhaa ya wazazi wake na ikiwa anataka kuolewa akiwa na miaka 14 itabidi apate ridhaa ya Mahakama na wakati huo huo Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 inaeleza wazi kwamba mwanaume yeyote atakayejamiiana na msichana chini ya umri wa miaka 18 atakuwa amebaka.

Hali kadhalika sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza kuwa mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Hivyo mgongano huu wa Sheria hizi unachangia kurudisha nyuma harakati za kulinda haki za wanawake kwa kuwa kwa

tafsiri ni kwamba mtoto anaweza pia kuolewa na kuitwa mama hali akiwa mtoto chini ya umri unaokubalika kuwa mtu mzima kwa mujibu wa sheria.

*9.6.2 Matumizi ya Sheria Zilizopitwa na Wakati*

Baadhi ya sheria zimekuwa ni kandamizi kwa wanawake. Hii inatokana na kwamba zilitungwa kwa kulenga mfumo dume. Sheria mojawapo ambazo ni kandamizi kwa wanawake ni Tamko la Sheria ya Kimila ya Mirathi ya Mwaka 1963. Sheria hii ilitungwa kutokana na mfumo dume kwani haimpi mwanamke nafasi ya kurithi au kumiliki mali alizochuma na marehemu mume wake. Pia haiwapi watoto wa kike wa marehemu nafasi ya kurithi au kumiliki mali aliyoiacha marehemu baba yao kama ilivyo kwa watoto wa kiume wanaoipata nafasi hii.

*9.6.3 Mila na Desturi Zilizopitwa na Wakati*

Masuala mengi kwenye jamii zetu yanaongozwa na mila na desturi. Kuzienzi mila na desturi sio kitu kibaya bali kuna mila na desturi zilizowekwa na waliiotangulia miaka mingi iliyopita ambazo zimekuwa zikitumika tangu enzi hizo ila kwa sasa zimepitwa na wakati; zilizingatia zaidi mfumo dume. Hivyo ni kwamba utawala na umiliki wa mali pamoja na maamuzi juu ya jambo lolote lile yalikuwa chini ya himaya ya wanaume. Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ambapo hadhi ya wanawake imekuwa ikitambuliwa katika jamii mbalimbali. Aidha baadhi ya jamii zimekuwa zikiendeleza mila na desturi zenye lengo la ukandamizaji dhidi ya wanawake; mila na desturi hizi zinalenga kumkandamiza mwanamke kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

Sheria pia inachangia kuendelea kuwepo kwa mila ambazo zina athari kwa wanawake ingawa siyo za moja kwa moja. Kwa mfano sheria ya Ndoa inapoipa Mahakama mamlaka ya kugawa mali kwa watalaka kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine, mila za wanandoa. Pia sheria inaelekeza Mahakama kuzingatia mila za wanandoa wakati wa kuamua mtoto akae na nani pale wanapotalikiana. Hivyo mahakama haikupaswa kuzingatia mila za wanandoa kwani kulingana na mila na desturi za makabila mengi ya Tanzania, upande wa mwanaume unakuwa na nguvu zaidi na hivyo ni rahisi kwa haki ya mwanamke kupotea.

*9.6.4 Uelewa Mdogo wa Sheria na Haki*

Wanawake wengi ambao pia ndio wahanga wakubwa wa masuala ya ukatili wa kijinsia hawana ufahamu juu ya sheria na misingi ya haki za binadamu na utawala bora. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imekuwa ni kikwazo kwa walio wengi katika kufuatilia kupata haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria.

*9.6.5 Mlolongo Katika Upatikanaji wa Haki*

Mlolongo katika upatikanaji wa haki huchangiwa na kesi mahakamani. Hali hii husababisha watu wengi kupoteza haki zao kutokana na mlolongo mkubwa wa taratibu za kimahakama pamoja na mamlaka nyingine zenye dhamana ya kuhakikisha kwamba haki ya mtu inapatikana . Kwa sababu hiyo inachangia watu wengi hasa wanawake kukata tamaa katika kufuatilia haki zao. Kutokana na usumbufu wanaoupata, wanawake hukata tamaa, hasa wanapokabiliwa na jambo/tatizo kwa mara nyingine, wengi wanaamua kubaki nalo pasipo kulitafutia ufumbuzi huku wakiendelea kuathirika kimwili, kiuchumi, kisaikolojia na kijamii.

*9.6.6 Umaskini*

Kutokana na umaskini wanawake wengi wanashindwa kutoka sehemu moja kwenda mahala pengine kwa ajili ya kutafuta haki zao ikiwa ni pamoja na kufika katika vyombo mbalimbali vinavyosimamia haki kama mahakama, polisi, mabaraza ya usuluhishi na vituo vya msaada wa kisheria. Pia wanawake wengi wanakosa fedha kwa ajili ya vitendea kazi wanapokuwa wanafuatilia haki zao kutokana na kukosa mahitaji muhimu kama karatasi kwa ajili ya kutolea nakala mbalimbali zinazokuwa zikihitajika na vyombo husika. Umasikini pia husababisha wanawake kupoteza haki zao kwa kukosa fedha za kuweka wakili au mwanasheria kwa ajili ya kusimamia shauri katika vyombo husika ikiwemo mahakama. Hata hivyo watu wachache hufika katika vituo vya msaada wa kisheria na kupata msaada wa kisheria. Vituo hivi mara nyingi vipo mijini tu ambapo watu wengi wanatoka vijijini inakuwa si rahisi kufika. Mbali ya vituo vya msaada wa kisheria kuwa mjini tu, pia kuna ukosefu wa mawakili wa kujitolea katika vituo vilivyopo hivyo watu wengi wanakosa haki zao kwa kukosa uwakilishi mzuri mahakamani.

*9.6.7 Ongezeko la Ukiukwaji wa Haki za Binadamu, Ukosefu wa Ulinzi na Rushwa*

Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la ukiukwaji wa haki za binadamu. Pia, kuna ukosefu wa makazi salama kwa wanawake ambao wanakuwa wamefanyiwa ukatili. Tatu, kuna tatizo sugu la rushwa ambayo imekuwa ni adui wa haki hasa kwa wanawake.




SURA YA

# 10

# Mapendekezo ya Jumla

# MAPENDEKEZO YA JUMLA

## 10.1 UTANGULIZI

Kuna haja ya kuimarisha mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia ili kuweza kuupunguza na hatimaye kuutokomeza kabisa. Kwa kufanya hivyo Tanzania itakuwa na jamii isiyo na ukatili na yenye ustawi wa raia wake na kukuza amani kwa maendeleo ya taifa. Hivyo basi wadau kutoka sekta mbalimbali wanawajibu wa kufanya yafuatayo;

## 10.2 MAPENDEKEZO KWA SERIKALI

a) Iridhie mikataba mbalimbali ya kimataifa inayolinda haki za wanawake na kuingiza kwenye sheria za nchi.
b) Irekebishe au ifute sheria kandamizi zilizopitwa na wakati.
c) Iweke mikakati ya kumuwezesha mwanamke kujikwamua kiuchumi kwa mfano, kwa kutoa mikopo ya riba nafuu.
d) Iingize somo la Haki za binadamu katika mitaala ya elimu.
e) Izingatie utekelezaji wa mikakati yake katika madawati ya jinsia katika wizara, taasisi zake kwa mfano dawati la polisi.
f) Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto iongezewe bajeti ili kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi.
g) Itengeneze makazi ya muda ya hifadhi ya wahanga wa ukatili wa kijinsia.
h) Itoe mafunzo ya sheria kwa watekelezaji wa sheria.
i) Itatue migongano iliyopo katika sheria katika kulinda haki ya mwanamke na mtoto kwa mfano, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto, Sheria ya Kazi.
j) Ihakikishe kuwa inatekeleza mipango ya kikosi kazi cha haki za wanawake.
k) Iandae programu maalum nchi nzima za kuwasaidia watoto wa kike walioacha shule kwa sababu mbalimbali.
l) Itoe dawa na vitendea kazi vya kutosha kwa wakunga wenye taaluma ya kuhudumia wanawake wajawazito.
m) Iunde mkakati maalum wa kufuatilia na kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia; na ukatili wa aina yoyote. Aidha itangaze ukatili wa kijinsia kuwa ni janga la kitaifa.
n) Itoe nafasi sawa kwenye nafasi za kufanya maamuzi kutoka kwenye asilimia 30 hadi kufikia asilimia 50 (50/50).

## 10.3 MAPENDEKEZO KWA TAASISI

a) Ziendelee kutoa elimu kwa jamii.
b) Ziendelee kuishauri serikali katika masuala ya sheria, haki za binadamu na ujasiriamali.
c) Zielekeze zaidi vijijini harakati za kupinga ukatili wa kijinsia.
d) Ziendelee kufanya ushawishi na utetezi wa mabadiliko ya sera na sheria mbalimbali.
e) Vyombo vya habari viendelee kuelimisha jamii juu ya madhara ya ukatili wa kijinsia.
f) Isimamie uundaji wa umoja wa kitaifa wa wanawake usiojali dini, elimu, siasa, kipato na kadhalika.

## 10.4 MAPENDEKEZO KWA JAMII

a) Jamiii ipige vita mila kandamizi dhidi ya wanawake
b) Jamii ibadili mtazamo kuhusiana na mila na desturi potofu dhidi ya wanawake.
c) Jamii iendelee kutoa taarifa kuhusiana na vitendo vya ukatili kwa mamlaka husika.

## 10.5 MAPENDEKEZO KWA WADAU WA MAENDELEO

Waendelee kuisaidia serikali, AZAKI na taasisi mbalimbali ili hatimaye kwa pamoja waweze kutokomeza ukatili wa kijinsia.

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AZAKi | Asasi Zisizo za Kiserikali. |
| Bw. | Bwana |
| CEDAW | Mkataba wa Kimataifa wa Kupinga Ubaguzi wa Aina Zote Dhidi ya Wanawake wa 1979. |
| CDC | Foram ya Utu wa Watoto |
| CHRAGG | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. |
| CIDA | Shirika la Kimaendeleo la Kanada. |
| CWCA | Kituo cha Msaada Kwa Wajane na Watoto. |
| FHI 360 | Afya ya Familia Kimataifa |
| HoP | Nyumba ya Amani |
| ICNIC TZ | Kituo cha Kimataifa na Mtandao wa Taarifa za Uhalifu. |
| KIKUHAMI | Kikosi cha Kutetea Haki za Mirathi. |
| KIU | Kampuni ya Kiswahili na Utamaduni |
| LEAT | Chama cha Wanasheria Cha Mazingira. |
| LHRC | Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Umaskini Tanzania. |
| NAGAAG | Shirika/Mtandao wa Kutetea Haki za Wanawake la Somalia. |
| NCA | Shirika la Misaada la Kanisa la Norway. |
| SACCOS | Chama cha Kuweka na Kukopa. |
| TALAPA | Chama cha Kulinda Ardhi. |
| TAWLA | Chama cha Wanawake Wanasheria. |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini. |
| UNFPA | Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu. |
| UNICEF | Shirika la Umoja wa Mataifa la Haki za Watoto. |
| UNIFEM | Mfuko wa Kimataifa kwa Ajili ya Maendeleo ya Wanawake. |
| USAID | Shirika la Misaada la Watu wa Marekani. |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI. |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| WiLDAF | Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika. |

ISBN 978-9987-9246-2-2